**KAMPUNI** za simu zatozwa faini ya mabilioni TCRA

UKURASA 5



**UCHIMBAJI** mchanga waishtua serikali, yaandaa tozo

UKURASA 3



**Messi aifikia rekodi ya Raul Ulaya**

UKURASA 21


# Nipashe

Alhamisi Februari 18, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580495

The Guardian digital

www.ippmedia.com


nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# NI PIGO

## VILIO, SIMANZI VYATAWALA, JPM, NDUGAI, LISSU, MABALOZI WANENA

UKURASA 2, 3, 4 NA 7





**MAALIM SEIF**

24/10/1943

17/02/2021

**MICHEZO** **JULIO: SABABU NGORONGORO HEROES KIPIGO KWA GHANA** UK. 23

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Zitto: Huu ni mtihani mzito kwetu

**Na Elizabeth Zaya**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema hakuna maneno ya kuelezea kuhusu uchungu walioupata kutokana na aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Maalim Seif Sharif Hammad.

Vilevile, amesema wamepata mtihani mkubwa wa kuondokewa na mwamba wa demokrasia Tanzania na mtetezi wa haki za wananchi.

Zitto alitoa kauli hiyo jana, alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam muda mfupi baada ya kutangazwa kwa kifo cha kiongozi huyo aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Hakuna maneno ambayo tunaweza kuyaeleza kwa wanachama, Wazanzibar na kwa Watanzania kwa ujumla kuhusiana na uchungu mkubwa wa taarifa hii, lakini sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.

"Kwa mujibu wa taarifa ya madaktari na leo (jana) asubuhi nilikuwa hospitalini mpaka saa mbili na nusu na nilionana na jopo la madaktari ambao walikuwa wanamhudumia mwenyekiti wetu, kiongozi wetu na baba yetu, na kwa hakika alikuwa anaonyesha matumaini ya kupata nafuu, lakini ilipofika majira ya saa tano akawa amerudi kwa muumba wake.

"Ninajua taarifa hii itakuwa imeleta mshtuko mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar, kwa wanachama wa ACT-Wazalendo Tanzania nzima na kwa Watanzania.

"Ninaomba kuchukua nafasi hii kuwafahamisha Watanzania kwamba Maalim Seif alitulea kiuongozi kwa namna ambayo tutaweza kuendeleza maono yake, fikra zake na nia yake ya kuiona Tanzania yenye demokrasia na Zanzibar ambayo Wazanzibar wanaishi kwa maridhiano," alisema.

Alisema taarifa za mipango ya mazishi watazitoa kwa umma baada ya mashauriano ya karibu kati ya chama hicho na serikali.

"Ninachukua fursa hii kama kiongozi wa chama, kuwaomba Wazanzibar, wanachama wa ACT-Wazalendo na Watanzania kuwa na utulivu katika kipindi hiki cha mtihani mkubwa sana kwetu cha kuondokewa na mwamba wa demokrasia ya Tanzania na mtetezi," Zitto alihitimisha.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitoa taarifa kwa wananchi ya kifo cha Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamad, Ikulu jijini Zanzibar, aliyefariki jana, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. **PICHA: IKULU**

# Ni pigo kifo cha Maalim Seif

**Na Waandishi Wetu**

NI pigo! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na kifo cha Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, kutokana na jitihada zake katika kuimarisha demokrasia na utawala wa haki nchini.

Taarifa za msiba huo wa kitaifa zilitangazwa jana mchana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambaye alitangaza siku saba za maombolezo kwa bendera kupepea nusu mlingoti.

"Maalim Seif Sharif Hamad amefariki leo Februari 17 mnamo majira ya saa 5:26 asubuhi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili alipokuwa akipatiwa matibabu," Rais Mwinyi alitangaza.

Dk. Mwinyi alitoa pole kwa familia ya marehemu na wananchi wa Zanzibar kwa msiba na kuondokewa na kiongozi huyo.

Baada ya kutangazwa kwa msiba huo, vilio vilianza kusikika maeneo mbalimbali ya Unguja huku mamia ya watu wakikusanyika katika makao makuu ya Chama cha ACT-Wazalendo eneo la Vuga.

Baadhi ya wanachama wa chama hicho walionekana kuwa na huzuni kubwa, wengine wakitokwa na machozi huku baadhi ya shughuli za kijamii zikisitishwa katika baadhi ya maeneo, ikiwa ni pamoja na maduka kufungwa.

Baada ya Rais kutangaza taarifa hizo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kitaifa ilikutana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kujadili na kupanga ratiba ya mazishi.

**SALAMU ZA JPM**

Kufuatia kifo hicho, Rais wa Tanzania, John Magufuli, alimtumia salamu za rambirambi Rais Mwinyi, huku akitangaza siku tatu za maombolezo.

Katika salamu hizo, Rais Magufuli alimwomba Rais Mwinyi kufikisha salamu za pole kwa familia ya Maalim Seif, Wazanzibar wote, wanachama wa ACT - Wazalendo, ndugu, jamaa na marafiki wote walioguswa na kifo hicho.

"Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Maalim Seif Sharrif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Ninatoa pole kwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dk. Mwinyi, familia, Wazanzibari, wanachama wa ACT-Wazalendo na Watanzania wote. Mungu amweke mahali pema peponi, Amina!" Rais Magufuli alisema.

Aliwataka wafiwa wote kuwa na moyo wa subira, uvumilivu na ustahimilivu katika kipindi hiki cha majonzi na kutangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa kuanzia jana na bendera zote zitapepea nusu mlingoti.

SPIKA NDUGAI

Spika wa Bunge, Job Ndugai, pia alimtumia salamu za rambirambi Rais Mwinyi kufuatia kifo cha Maalim Seif, akisema: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Maalim Seif Sharrif Hamad, na kwa niaba ya Bunge, ninatoa pole kwa familia ya marehemu, Rais wa Zanzibar, Chama cha ACT-Wazalendo, Wazanzibar na Watanzania wote.

"Taifa limempoteza kiongozi mahiri ambaye alitumia muda wake mwingi katika kuwatumikia wananchi na kwa hakika mchango wake katika kuleta maendeleo, kudumisha amani na umoja wa kitaifa visiwani Zanzibar utakumbukwa daima."

**WACHAMBUZI, WANASIASA**

Abdulkarim Atik, mchambuzi wa siasa, alimzungumzia Maalim Seif, alisema jana kuwa alikuwa na mchango mkubwa katika kuboresha uhusiano wa kudumu kati ya Zanzibar na mataifa ya nje.

"Katika Visiwa vya Ngazija, aliboresha uhusiano wa Zanzibar na hata nchi nyingine. Pia, nchi za Falme za Kiarabu alitumia turufu yake wakati Mzee Mwinyi akiwa Rais, na kufanya biashara kati ya visiwa hivyo na Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kuboreka," alisema na kusifu mchango wa kiongozi huyo katika kuimarisha diplomasia na kukuza uchumi.

"Kwake ilikuwa ni sifa ya kiongozi kwanza tofauti na vijana hivi sasa wanaangalia uongozi una mshahara gani," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha ADC, Hamad Rashid Muhammed, alisema Maalim Seif alikuwa mpigania haki za binadamu na misingi ya utawala bora tangu akiwa kiongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) alikofukuzwa na Mwalimu Julius Nyerere.

Alisema Maalim Seif alifukuzwa ndani ya CCM na wenzake kutokana na msimamo wake wa kutetea maslahi ya Zanzibar katika mfumo wa Muungano pamoja na maslahi ya Wazanzibar katika serikali.

"Kwa mara ya mwisho Maalim Seif alinitaarifu kuwa anaumwa na nimwombee dua kupitia mawasiliano yetu ya ujumbe wa simu," alisema Hamad Rashid ambaye alikuwa miongoni mwa waasisi wa CUF kabla ya kufukuzwa na uongozi wa Maalim Seif na kuanzisha chama chake cha ADC.

Mwanasiasa na mwandishi mkongwe Zanzibar, Ali Saleh, alisema alama kubwa aliyoiacha Maalim Seif na itakayoendelea kukumbukwa Zanzibar, ni kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Alisema Maalim Seif alikuwa mwanasiasa mwenye tabia na moyo wa uvumilivu na ndiyo maana ameivusha Zanzibar na kubaki katika amani na umoja wa kitaifa licha ya kuibuka migogoro ya uchaguzi tangu mwaka 1995.

"Hakuna kiongozi mwenye uvumilivu kama Maalim Seif, sote tunafahamu uchaguzi wa Zanzibar ulivyokuwa ukifanyika, lakini alikuwa mvumilivu na kudumisha amani na umoja wa kitaifa kwa maslahi ya Zanzibar," alisema.

Mshauri wa ACT-Wazalendo, Juma Said Sanani, alisema kuna mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa Maalim Seif ikiwamo tabia yake ya kuwa mvumilivu kila matatizo ya kisiasa yanapojitokeza.

Alisema kifo cha Maalim Seif kimeacha pengo kubwa kwa ACT-Wazalendo, lakini amejitahidi kutengeneza wanasiasa wazee na vijana na wanaamini kuwa yupo mtu ana uwezo wa kuvaa viatu vyake.

Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Vuai Ali Vuai, alisema mchango wa Maalim Seif katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni mkubwa na hautasahaulika kwa sababu maridhiano ya kwanza yalifanyika mwaka 1999.

Alisema majadiliano mengine ya mwafaka ni ya mwaka 2007 na hatimaye jitihada zikazaa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

"Kwa kweli tumeondokewa na kiongozi wa kitaifa, ni pengo kubwa. Nichukuwe nafasi hii kuwapa pole ACT, wanafamilia na Wazanzibar wote, sote kwa pamoja tungane kumwombea dua Mungu amweke pahala pema peponi," alisema.

**●Imeandikwa na Rahm Suleiman (ZANZIBAR) na Christina Mwakangale (DAR)**

HABARI KITAIFA

# NGO zatakiwa kuzingatia sheria za nchi

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

SERIKALI imezisisitizia asasi za kiraia nchini kuzingatia sheria na taratibu zilizopo katika mchakato wa kuandaa na kupitisha ripoti za masuala ya haki za kibinadamu nchini kwa kutoa taarifa halisi ya mambo yanayotendeka.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, alisema hayo jana wakati akifungua kikao cha tathmini ya kuandaa ripoti ya pamoja ya namna Tanzania inavyotekeleza haki za binadamu itakayowasilishwa kwenye Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu.

Alisema taarifa hiyo izuie lugha isiyofaa na mambo yote ambayo yamekatazwa na kwamba serikali itaendelea kushirikiana na asasi hizo.

Mpanju alizipongeza asasi hizo za kiraia kwa umoja zilizoonyesha kwa kuandaa taarifa ya pamoja hali inayoonyesha ukomavu na uzalendo mkubwa, bila kujali kuwa wanafanya kazi katika maeneo yenye maudhui tofauti.

"Inaonyesha kwanza ushirikiano miongoni mwenu ni mkubwa, lakini mmejua kwamba mkiwa pamoja mtapeleka taarifa ambayo imejumuisha wananchi wote kupitia mlango wa AZAKI. Lakini itawapa fursa ya kupata ushahidi dhahiri kutoka kwa wahusika kwa mujibu wa kanuni za uandishi wa taarifa ambazo hazitakiwi kuwa na lugha ya isiyofaa," alisema Mpanju.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema pamoja na kuwapo utekelezaji wa kupambana na rushwa sambamba na kutokomeza mauaji ya watu wenye ulemavu, ripoti zinaonyesha kwamba haki za watoto zimekuwa zikivunjwa kila siku.

Pia alisema wamekutana zaidi ya asasi 100 ili kupitisha ripoti maalum ya haki za binadamu pamoja na kweda Umoja wa Mataifa kuangalia hali ya Tanzania inavyoheshimu na kulinda haki za binadamu.

Naye Kamishna wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Dk. Fatuma Khalfan, alipongeza juhudi za serikali katika kutekeleza mapendekezo yaliyoridhiwa tangu tathmini ya kwanza ya mwaka 2008.

Mjumbe wa Bodi ya Watetezi wa Haki za Binadamu, Keneth Simbaya, alisema masuala ya haki za binadamu ni muhimu hususani katika mustakabali wa nchi kwa kuleta usawa, kuheshimu utu na kuhakikisha kila mtu anaiona Tanzania ni mahali salama pa kuishi.

Alisema wamekubaliana kuwa mambo wanayoyaripoti yawe katika uhalisia wake na kwamba wanaangalia nini kimefanyika, nini hakijafanyika na changamoto gani zilizosababisha kisifanyike. Aliongeza kuwa katika kutekeleza haki za binadamu ni vyema kuhakikisha kila mtu anazifurahia.




Maalim Seif Sharif Hamad, akionyesha kadi ya uanachama wa Chama cha ACT- Wazalendo, baada ya kukabidhiwa na kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe (wapili kulia), siku alipojiunga rasmi na chama hicho. **PICHA: MAKTABA**

# Mabalozi, Lissu wamlilia Maalim Seif

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya viongozi wa kisiasa, mabalozi, mawaziri na waliokuwa wabunge, wamezungumzia kifo cha Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharrif Hamad, wengi wakisema alikuwa kiongozi shupavu.

Katika ukurasa wake wa Twitter jana, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, aliandika: "Kwa masikitiko makubwa, ninatuma salamu za rambirambi kwa familia, wana ACT-Wazalendo, Wazanzibar na Taifa kwa ujumla juu ya kifo cha Maalim Seif Sharrif Hamad."

Lissu aliyewania urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, alisema Maalim Seif alikuwa kiongozi mwenye ushawishi na mtetezi wa haki ya Wazanzibar.

Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, alisema: "Ninaungana na Watanzania hasa Wazanzibar katika kipindi hiki cha majonzi ya kuondokewa na Maalim Seif ambaye amekuwa kwenye siasa kwa zaidi ya miaka 40.

"Amekuwa kielelezo cha kiongozi mtumishi anayewaweka watu mbele kabla ya madaraka. Hatuwezi kuziba pengo lake lakini tunapaswa kuheshimu urithi aliotuachia."

Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Dannell, aliandika: "Salamu zangu za rambirambi ni kwa familia na marafiki wa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Maalim Seif. Kujitoa kwake kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar na jitihada zake katika demokrasia na amani vitakosekana. Nitamkumbuka kwa dhamira na huruma yake."

Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) - Tanzania liliandika katika ukurasa wake wa Twitter jana: "Tunatoa pole kwako Rais John Magufuli, Rais wa Zanzibar, Watanzania wote na familia ya Hayati Maalim Seif kwa msiba huu mkubwa kwa taifa."

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, aliandika: "Nikiwa hapa Dubai UAE, nimeshtushwa na taarifa za kutwaliwa kwa Mheshimiwa Sharrif Hamad, Jabali la Mageuzi Tanzania, Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo na Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar.

"NInatoa pole nyingi kwa familia, chama chake, Wanzanzibar na Watanzania wote. Kwake tumetoka na kwake tutarejea."

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, aliandika: "Pumzika kwa amani Mzee wetu Maalim Seif, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Ninatoa pole kwa familia, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Watanzania wenzangu wote."

Aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini (CHADEMA), Godbless Lema, alisema: "Maalim Seif alikuja kunisalimia nilipokuwa mahabusu, alinitia moyo, aliniambia mawazo imara na fikra thabiti juu ya ukombozi yanapatikana jela.

"Alinieleza kwa kifupi safari yake ndani ya gereza enzi zake. Ninawapa pole familia na chama chake, tuchukue tahadhari."

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema "Mwamba wa demokrasia na siasa za vyama vingi Tanzania umetuacha na deni kubwa kama vijana. Deni la uzalendo, misimamo na mshikamano. Nenda salama, Mungu akusamehe madhambi yako yote na akupe rehema ya milele."

●**Imeandikwa na Salome Kitomari na Maulid Mbaga**

# Uchimbaji mchanga waishtua serikali

**Na Mwandishi Wetu, BAGAMOYO**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, amesema iko haja kuweka tozo maalum ya kurejesha hali ya mazingira kutokana na athari za uchimbaji wa mchanga katika maeneo ya Bagamoyo mkoani Pwani.

Akikagua maeneo ya uchimbaji wa mchanga katika Kitongoji cha Kitopeni, Kata ya Kiromo wilayani Bagamoyo jana, Waziri Ummy alisema suala la uhifadhi na usimamizi wa mazingira ni jukumu la kila mwananchi.

Ummy alisema ni wajibu wa wachimbaji wa mchanga kuwa na mpango wa kurejesha mazingira katika hali yake ya awali baada ya kumaliza shughuli za uchimbaji kama ilivyo kwenye uchimbaji wa madini.

"Tunataka kuona mwekezaji anatekeleza mpango wa kurejesha mazingira katika hali yake ya awali baada ya shughuli za uchimbaji kukamilika," alisema.

Waziri huyo alisema uchimbaji wa mchanga uendane na hifadhi ya mazingira na kusisitiza azma ya serikali kulinda afya za watu wake na mazingira yanayowazunguka.

Pia, aliitaka jamii ya Pwani kuhakikisha inatunza mikoko kwa manufaa ya mazingira ya bahari na bioanuai kwa kubuni chanzo mbadala cha mapato na kutolea mfano ulimaji wa kilimo cha mwani badala ya ukataji wa mikoko kwa matumizi ya kuni na mkaa, akiipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kupanda ekari 22 za mikoko kupitia mradi wa TASAF.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa, alisema biashara ya uchimbaji mchanga ni chanzo kikubwa cha mapato katika halmashauri yao na kusisitiza umuhimu wa kuboresha mazingira ili kuwa shughuli endelevu za uchimbaji mchanga.

"Ipo haja ya kuainisha maeneo ya kuchimba mchanga na si kila eneo ni sahihi kwa uchimbaji," Kawawa alisema.

Akiwa katika siku ya pili ya ziara ya kukagua shughuli za utunzaji na uhifadhi wa mazingira mkoani Pwani, Waziri Ummy jana alitembelea Kitongoji cha Kitopeni, Kata ya Kiromo pamoja na vitongoji vya Kondo na Mlingotini.

# Hivi ndivyo atakavyokumbukwa Maalim Seif

Na Mwandishi Wetu

JABALI limeanguka. Ni maneno yanayoweza kuelezea undani wa kifo cha mwanasiasa nguli wa Tanzania, Maalim Seid Sharif Hamad.

Maalim Seif alifariki dunia jana katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) alikokuwa akipatiwa matibabu tangu alipolazwa Januari 31, mwaka huu. Hadi anakumbwa na mauti, alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) iliyo chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Kutokana na historia yake kisiasa na uongozi, anaweza kuitwa jabali. Atakumbukwa kwa mambo mengi katika historia ya Tanzania na uongozi ndani ya vyama vya siasa na serikali kwa ujumla. Ni vigumu kuitaja Zanzibar bila kumhusisha Maalim Seif.


Maalim Seif ametangulia mbele za haki, lakini atakumbukwa ndani na mipaka ya Tanzania kutokana na mambo mengi aliyoyafanya zaidi ya miaka 40 tangu alipoingia katika siasa na uongozi. Miongoni mwa mambo ni kama ifuatavyo;-

KUPANDA NA KUSHUKA

Tofauti na wanasiasa wengine, Maalim Seif, kama alivyokuwa anajulikana, amevuka mito, milima na mabonde katika maisha yake. Ni mtu ambaye alikuwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na kuondolewa kutokana na joto la kisiasa Zanzibar.

Pia alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Katibu wa Uchumi na Mipango, lakini alifukuzwa uanachama wakati wa mfumo wa chama kimoja.

Pamoja na hayo yote, hakutikisika wala kuhamanika licha ya kwamba baadaye aliwekwa kizuizini kwa sababu za kisiasa.



### KUASISI MAGEUZI

Kutokana na kuingia kwa mfumo wa vyama vingi mwanzoni kwa miaka ya 1990, Maalim Seif alikuwa mmoja wa wanasiasa walioasisi vyama vingi huku akiwa mmoja wa wanasiasa walioanzisha Civic United Front (CUF). Wanasiasa wengine walioanzisha chama hicho ni Shaaban Mloo, James Mapalala, Rashid Hamad Mohamed, Juma Duni Haji na Ali Mazrui.

Maalim Seif alichaguliwa kuwa makamu mwenyekiti huku Mapalala akiwa Mwenyekiti na Mloo Katibu Mkuu. Baadaye Mapalala alifukuzwa uanachama na nafasi yake kuchukuliwa na Mzee Musobi Mageni Musobi kabla ya Prof. Ibrahim Lipumba kuchukua nafasi hiyo.

### UVUMILIVU KISIASA

Pamoja na kuondolewa katika uongozi, kukumbwa na dhoruba za kisiasa na kufukuzwa uanachama CCM, Maalim Seif aliendelea kuwa 'ngangari' (kuhimili vishindo) kama alivyokuwa akitumia neno hilo ndani ya CUF.

Licha ya kuhimili hilo, Maalim Seif aliweka rekodi ya kuwa mgombea urais Zanzibar tangu kufanyika kwa uchaguzi uliohusisha vyama vingi vya siasa. Mwaka 1995 uchaguzi ulipofanyika kwa mara ya kwanza, alichuana na Salmin Amour Juma.

Katika uchaguzi huo, alishindwa kwa kukupata asilimia 49.76 dhidi ya Salmin aliyepata asilimia 50.26. Pamoja na kushindwa kwa kiwango hicho kidogo, Maalim Seif alidai kuwa alikuwa mshindi, lakini alipokwa haki yake.

Maalim Seif aligombea tena urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 na kupata asilimia 31.96 ya kura zilizopigwa huku Amani Abeid Karume aliyapata asilimia 67.04. Matokeo hayo kama yalivyokuwa ya mwaka 1995, yalipingwa na CUF kwa madai kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa sheria na taratibu za uchaguzi pamoja na wizi wa kura.

Matokeo hayo yalisababisha tena mpasuko wa kisiasa na hata baadhi ya wafuasi wa CUF kutiwa matatani kwa madai ya kutokuheshimu sheria na kutokutii amri halali za vyombo vya dola.

Kutokana na viongozi na wanachama wa CUF kuendelea kutokuyakubali matokeo hayo, kulifanyika maandamano Januari 26 na 27, 2001 yaliyosababisha wanachama na wafuasi 45 wa chama hicho kupoteza maisha kwa madai ya kupigwa risasi na vyombo vya usalama.

Maalim Seif aliendelea kuwania urais kupitia CUF katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 30, 2005. Azma yake ya kuingia Ikulu iligonga mwamba baada ya kushindwa tena dhidi ya Karume. Maalim Seif alipata asilimia 46.07 dhidi Ya Karume aliyepata asilimia 53.18.

Kutokana na matokeo hayo, CUF walipinga na kuweka msimamo wa kumtambua Karume kama Rais kwa madai kwamba uchaguzi ulitawaliwa na ukiukwaji wa sheria kama ilivyokuwa kwa ule uliopita.

Uchaguzi wa mwaka 2010 haukuwa tofauti kwa matokeo kama ule wa miaka ya nyuma. Maalim Seif aligombea kwa mara nyingine akichuana na Dk. Ali Mohamed Shein. Katika matokeo yaliyotangazwa Novemba Mosi, 2010 Dk. Shein alitangazwa mshindi kwa kupata kura 179,809 sawa na asilimia 50.1 huku Maalim Seif akipata kura 175,338 (asilimia 49.1).

Hata hivyo, katika uchaguzi huo hakukuwa na malalamiko kutokana na makubaliano yaliyosababisha kufanyika kwa mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kuhusu kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Katika makubaliano hayo, ilikubaliwa pamoja na mambo mengine kwamba chama kitakachopata asilimia 15 ya kura kitashiriki kuunda SUK, hivyo kwa kura hizo, Maalim Seif alikuwa na uhakika wa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na baadhi ya wanachama wake kuingia kwenye serikali.

Mwaka 2015 aligombea kwa mara ya tano huku akichuana tena na Dk. Shein na hatimaye matokeo yalifutwa baada ya Maalim Seif kujitangaza mshindi. CUF iligoma uchaguzi wa marudio na hatimaye kushindwa kushiriki kuundwa kwa SUK.

Mwaka jana ilikuwa mara nyingine kwa Maalim Seif kugombea urais wa Zanzibar safari hiyo akipambana na Dk. Ali Hassan Mwinyi aliyetangazwa mshindi. Matokeo ya uchaguzi yalilalamikiwa, lakini baadaye wawili hao walikaa na kufikia makubaliano yaliyowezesha kwa mara nyingine kuundwa kwa SUK.

Kutokana na makubaliano hayo, Maalim Seif, aliteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais, nafasi aliyoishika mpaka kifo chake.

### MZEE WA MWAFAKA

Pamoja na kuwapo kwa mpasuko wa kisiasa Zanzibar, Maalim Seif dhahiri alionekana alikuwa akipenda amani na utulivu. Kutokana na ukweli huo, alishiriki mazungumzo ya mara kwa mara hasa baada ya uchaguzi wa mwaka 1995 na ule wa mwaka 2000 kwa lengo la kufanikisha hilo.

Hatua hizo zilizaa makubaliano yaliyopewa jina la Mwafaka I ulitiwa saini Juni, 1999 kutokana na mazungumzo yaliyosimamiwa na wazee wenye hashima pamoja na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Chifu Emeka Anyaoku, aliyewakilishwa na Dk. Moses Anafu.

Pia alishiriki mwafaka wa pili pili ulioshirikisha wazee, viongozi wa CUF na CCM wakiongozwa na makatibu wakuu Maalim Seif (CUF) na Philip Mangula kwa upande wa CCM.

Mwafaka huo ulikuwa wa kihistoria kwani pande hizo zilifikia makubaliano ya mambo mbalimbali ikiwamo kuwamo kwa wabunge na wawakilishi wa kuteuliwa kutoka CUF. Mmoja wa walioteuliwa kuwa wabunge ni Hamad Rashid Mohamed.

Aidha, mwafaka huo uliipa sifa Tanzania kwani Mangula na Maalim Seif walipata mialiko mbalimbali ya kimataifa kwenda kuelezea ni njia gani walizotumia kutatua mgogoro wa kisiasa bila kutumia watu wa nje.

### MWASISI WA SUK

Baada ya miaka mingi ya misigano ya kisiasa Zanzibar, hatimaye Maalim Seif na Karume walikaa na kujaribu kumaliza tofauti za kisiasa Zanzibar ambazo pamoja na mambo mengine, walikubaliana kuanzishwa kwa SUK.

Katika kufikia huko, walikubaliana kufanya marekebisho ya Katiba ya Zanzibar yaliyowezesha kuwapo kwa SUK.

# HABARI KITAIFA

## Mkandarasi matatani madai ya kutoza wananchi fomu umeme

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKANDARASI wa Kampuni ya Edward General Electrical, ametiwa matatani na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwa tuhuma za kuwatoza wananchi wanaohitaji kuunganishiwa umeme jijini hapa.

Hatua hiyo imechukuliwa ikiwa ni siku chache baada ya TAKUKURU kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Dodoma, kuanza kusikiliza kero za rushwa kwa wananchi.

Mkandarasi huyo anadaiwa kuwatoza Sh. 25,000 wananchi 33 wa Kata Ng'ong'ona jijini hapa kwa ajili ya fomu za kuunganisha umeme katika nyumba zao. Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema jana kuwa wananchi hao wametozwa fedha hizo licha ya fomu hizo kutolewa bure na TANESCO.

"Usikilizaji kero hizi ulianza Februari Mosi, mwaka huu, ilitokana na malalamiko ya uwapo wa vitendo vya rushwa kwenye uunganishaji umeme kwenye makazi ya wananchi," alisema.

Kutokana na kujiridhisha kuwa amefanya hivyo, alimtaka mkandarasi huyo kurudisha fedha hizo kabla ya TAKUKURU haijamfikia.

"Tunaendelea kufuatilia suala hili ili wananchi wapate haki zao. TAKUKURU inamtafuta mkandarasi ili arejeshe fedha hizi kwa wananchi waliolipishwa isivyo halali," alisema.

"Tunaendelea kufuatilia suala hili na kuhakikisha fedha hizo zinarudi kwa wananchi kwa sababu TANESCO wamesema fomu hizo hutolewa bure," alisisitiza. Sambamba na hilo, aliwataka viongozi wa kata na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi kabla ya kukubali kutozwa fedha kwa ajili ya malipo ya maendeleo wanayotaka kufanya.

Kibwengo alisema wananchi wengi wamekuwa wakitozwa fedha bila kujua ni za nini.



Baadhi ya waumini wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha la Mt. Theresia wa Mtoto Yesu, wakipakwa majivu katika paji la uso kanisani hapo jana, wakati wa ibada ya Jumatano ya Majivu ambayo ni mwanzo wa kipindi cha Kwaresma. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## TCRA yatoza kampuni za simu faini mabilioni

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imezipiga faini ya zaidi ya Sh. bilioni 38 kampuni sita za simu baada ya kupima ubora wa huduma zinazozitoa.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Mhandisi James Kilaba, akizungumza jana na waandishi habari Dar es Salaam jana, alisema faini hizo zimepatikana baada ya TCRA kupima ubora na kubaini matatizo katika maeneo 11.

Mhandisi Kilaba alisema fedha hizo za faini wanatakiwa waziweke katika akaunti zao kwa ajili ya kuboresha huduma za mawasiliano ndani ya miezi mitatu.

"Upimaji wa huduma za mawasiliano kwa kampuni sita za simu za mkononi ulifanyika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Singida, Kilimanjaro, Mbeya, Unguja, Tanga na Simiyu kwa kuangalia vigezo mbalimbali," alisema.

Alitaja faini zilizopigwa kwa kila kampuni ni Airtel Sh. bilioni 11.5, Tigo Sh. bilioni 13, Halotel Sh. bilioni 3, Vodacom Sh. bilioni 7.8, ZANTEL Sh. bilioni 1 na TTCL Sh. bilioni 1.

Mhandisi Kilaba alitaja maeneo waliyopima ni kiwango cha simu zilizoshindikana kuunganishwa, kiwango cha simu zilizo katika muda wa kuunganisha simu iliyopigwa na wigo wa upatikanaji wa huduma.

Pia alisema waliangalia kiwango cha simu zilizofanikiwa kuunganishwa, kiwango cha uwezo wa minara kupokezana mawasiliano, wastani wa muda unaotumika katika kupakia na kupakua takwimu (data), uwiano wa muunganisho wa data, pamoja na upatikanaji wa huduma za jumbe fupi.

Alisema kwa mujibu wa kanuni ya 20 ya kanuni hizo, mtoa huduma atakayeshindwa kufikia vigezo vya ubora wa huduma anawajibika kulipa faini za viwango mbalimbali.

Pia alisema kutokana na faini hiyo, kila mtoa huduma anatakiwa kuwasilisha mpango kazi wa kimaandishi TCRA ndani ya siku tatu wa namna atakavyotumia fedha hizo za faini katika kuboresha huduma zake kama alivyoelekezwa.

## Ndejembi akemea mazoea utumishi wa umma

**Na Mwandishi Wetu,**
MPWAPWA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewataka watumishi wa umma kuwa na mpango kazi utakaomwezesha kila mmoja kufanya kazi kwa ufanisi na utoaji huduma bora kwa umma.

Ndejembi alitoa maelekezo hayo jana wakati wa ziara yake ya kikazi katika wilaya za Mpwapwa na Kongwa mkoani Dodoma. Alisema ni jukumu la waajiri kuhakikisha kila mtumishi anatekeleza mpango kazi wake ili kutoa mchango wa kiutendaji mahali pa kazi badala ya kuendelea kufanya kazi kwa mazoea, jambo ambalo alisema halina tija katika maendeleo ya taifa.

Sambamba na hayo, Ndejembi aliwasisitiza watumishi wa umma kuzingatia ujazaji wa fomu za mfumo wa wazi wa mapitio na tathmini ya utendaji kazi (OPRAS) ili kutoa fursa kwa waajiri kupima utendaji kazi wa watumishi wao kwa lengo la kuwapa stahiki kulingana na utendaji kazi wao.

"OPRAS ipo kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira ya Mwaka 1998 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2008 pamoja na Sheria ya Utumishi Sura Namba 298, hivyo ni jukumu la waajiri kuhakikisha watumishi wanajaza fomu na kufanyiwa tathmini ya utendaji kazi wao ili kuongeza ufanisi kiutendaji," alisisitiza.

Akijibu hoja ya Kandindo Mumeli, mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kuhusu baadhi ya waajiri kutotenga bajeti ya kuwahudumia watumishi wa umma wenye ulemavu kama Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma wenye Ulemavu wa Mwaka 2008 unavyoelekeza, Ndejembi aliwataka waajiri kutoa kipaumbele kwa kutenga fedha za kuwahudumia watumishi hao ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Pia alisisitiza juu ya usimamizi wa ruzuku inayotolewa na serikali kwa wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

Alisema ni jukumu la kila mtumishi wa umma kuhakikisha fedha wanazopokea wanufaika wa mpango huo unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAFO zinatumika kuboresha maisha yao kwa kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo.

"Kumekuwa na mtazamo hasi juu ya usimamizi wa fedha za TASAF kuwa ni jukumu la waratibu wa TASAF pekee, jambo ambalo halina tija kwa taifa kwani usimamizi wa fedha za umma ni jukumu la kila mtumishi. Ni wajibu wetu sote kuhakikisha fedha za umma zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa," alisema.

Ndejembi pia alipiga marufuku kitendo cha kukata fedha za wanufaika wa TASAF, ili kuchangia Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kwa kuwa kitendo hicho kinawakwamisha wanufaika kutumia ruzuku waliyopewa katika shughuli mbalimbali za maendeleo zitakazoboresha maisha yao.

Ndejembi aliongeza kuwa wanufaika wa TASAF waachwe huru kutumia ruzuku wanazopatiwa katika shughuli mbalimbali za maendeleo ili watakachozalisha ndicho wakitumie kuchangia CHF kwa hiari.


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA

ILIYOPO DAR ES SALAAM

SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 535/16 YA 2017

VODACOM TANZANIA PLC ........................................ MWOMBAJI

DHIDI YA

INNOCENT DANIEL NJAU ........................................ MJIBU MAOMBI

KWA:

INNOCENT DANIEL NJAU
POPOTE ULIPO.

Unajulishwa kwamba shauri la maombi ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa tarehe 19/3/2021 saa tatu kamili asubuhi (3:00) Mahakama ya Rufani, Dar es Salaam.

Unatakiwa kufika bila kukosa mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria.

Elewa kuwa usipofika wewe au mwakilishi wako, shauri hili litasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa hii leo tarehe 2 Mwezi Februari, 2021.

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

B. A. Mpepo
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mjadala sekta ya maji muhimu sasa

**MOJA** ya sekta inayogusa maisha ya wananchi wengi kila siku ni ya maji. Hii ni kutokana na umuhimu wake katika maisha ya watu na viumbe wengine, na bila maji dunia haitakuwa mahali salama pa kuishi.

Kutokana na umuhimu huo, tunaweza kusema kwamba bila maji hakuna maisha.

Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kumekuwa na kupungua kwa kiwango cha maji ardhini, kiasi cha kuongeza migogoro kati ya binadamu na binadamu, wanyama na binadamu hasa katika maeneo ya ufugaji na yaliyohifadhiwa.

Lengo la serikali ni kusambaza maji kwa wananchi na yapatikane umbali usiozidi mita 400, ili kuhakikisha hawapotezi muda mrefu katika kutafuta maji na kuwapatia majisafi na salama.

Kwa muda mrefu, sekta hiyo haijatulia kutokana na kwamba miradi mingi ya maji imeshindwa kusimama kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo miradi iliyokamilika, lakini haijatoa maji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Baadhi ya maeneo wataalamu walipima ardhi na kuona kuna maji ya kutosha na baada ya kuchimba maji hutoka kwa muda fulani na baadaye kupungua na kupotea kabisa, kiasi cha mradi kuonekana hewa.

Juzi Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza kutenguliwa uteuzi wa viongozi 22 wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kutokana na kuonyesha udhaifu wa kiutendaji na kusababisha utekelezaji miradi ya maji kusuasua.

Kusuasua kwa miradi mingi kumesababisha wananchi kukosa majisafi na salama, ambayo huwasaidia kuwaepusha na majanga mbalimbali ikiwamo kuugua magonjwa ya nlipuko kama matumbo na mengine ambayo huwarudisha nyumba kimaendeleo.

Kukosekana kwa maji kumepelekea wanawake na watoto kutembea umbali mrefu kusaka maji kiasi cha kusababisha wengine kubakwa, kupata matatizo ya kiafya na kushindwa kutekeleza shughuli za maendeleo.

Malalamiko za miradi ya maji kutotekelezwa kwa viwango na kusuasua ni kikubwa, kiasi cha kusababisha hatua mbalimbali kuchukuliwa huku, kelele za wananchi zikiwa nyingi, lakini bado tatizo limeendelea.

Miradi ya maji hugharimu mabilioni ya fedha na inapotokea haikukamilika au kuwa hewa ni kilio na maumivu makubwa kwa walipakodi ambao matamanio yao ni kuona kodi inafanya jambo la maendeleo.


Ndiyo maana tunaona kuna umuhimu sana wa kuwa na mjadala wa kitaifa ambao utawaleta pamoja wadau wa maji ili kuwa na mwelekeo mmoja wa kushughulikia miradi ya maji iwe endelevu.

Lakini ili kuwe na maji, ni lazima kuwe na mazingira mazuri yaliyotuzwa ikiwamo kupanda miti, na ni muhimu pia Wizara ya Maji ikashirikiana na Wizara ya Mazingira kuhakikisha kasi ya upandaji miti na kutunza mazingira inaongezeka, ikiwamo kutunza vyanzo vya maji na kutekeleza sheria ya kutojenga ndani ya chanzo cha maji.

Aidha, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inalenga kuboresha huduma za maji vijijini kufikia asilimia 95 ifikapo 2025, huku malengo ya kati ni kuboresha huduma ya maji vijiji kwa asilimia 85 hadi mwaka jana.

Vijijini ndiko kuna idadi kubwa ya watu, na iwapo kutakuwa na majisafi na salama, huduma za miundombinu, afya na elimu hakutakuwa na haja ya watu kukimbilia mjini kupata unafuu wa maisha. Tunaona ni muhimu mjadala wa mara kwa mara wa wadau wa maji ukafanyika ili kuhakikisha miradi inakuwa endelevu na yenye tija kwa wanufaika wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ni kweli tunakiri ajali haina kinga, pia kuna...

Na Sabato Kasika

**NENO** ajali linatajwa kuwa tukio lenye sifa mbili; linalojulikana na lisilotarajiwa. Hilo linatokea katika muda na mahali fulani, bila ya kuwapo sababu au makusudi na unasababisha madhara mengi, kwa watu ikiwamo vifo na hata ulemavu wa kudumu.

Ajali zikiwamo za magari, moto na nyingine nyingi, ni matokeo mabaya, ambayo wakati mwingine yanaweza kuepukwa au kukingwa, ikiwa matukio yaliyosababisha yangetambuliwa na kurekebishwa kabla ya tukio hilo.

Katika lugha ya Kiswahili, kuna methali 'ajali haina kinga' na imekuwa ikitumiwa na watu wengi, kwa kuwa wanaamini kwamba, hakuna mtu anayeweza kuzuia ajali pale inapotokea.

Hilo ni kweli kwamba, yasiyozuilika kuhusu ajali, lakini kuna haja kwa kila mtu kuchukua hatua zaidi katika matumizi ya methali hiyo ili kuepuka ajali ambazo zinaweza kuwa ndani ya uwezo wake.

Kwa mfano, ni marufuku kwa magari kuingia kuhudumiwa kujaza mafuta katika vituo vyake, kwa sababu ni hatari kwa vyombo hivyo vya usafiri na abiria wake, ambao ndio mahsusi walengwa.

Hiyo ina mana kwamba, panapotokea mlipuko wa moto wakati gari linajaza mafuta huku lina abiria, kuna uwezekano mkubwa wa watu kupoteza maisha, kutokana na ajali ambayo ingeweza kukingwa.

Ikumbukwe, ni muda mrefu tangu serikali ipige marufuku magari ya abiria kujaza mafuta abiria wakiwamo, lakini hadi sasa baadhi ya madereva na wasaidizi wao hawatii maelekezo hayo.

Pindi inapotokea kwamba, gari linapata moto, ni wazi methali hiyo ya 'ajali haina kinga' itakuwa haina uzito, kwa kuwa tayari inakiukwa marufuku iliyokwishatangazwa; hakuna gari ya abiria inapaswa kujaza mafuta mahali hapo na abiria wakiwamo,

Ni suala la umakini tu linalotakiwa kuzingatiwa, ili kuepusha ajali zisizo za lazima, ikiwamo hali inayoweza kusababishwa na uzembe wa madereva, wasaidizi wao, abiria na hata wafanyakazi wa vituo vya mafuta.

Umefika wakati sasa, abiria waaamke na kupaza sauti ya kuwazuia madereva wanaoenda sheli kujaza mafuta, kwa kuwa hiyo ni njia mojawapo ya kujinusuru, badala ya kunyamaza tu na kuamini katika 'ajali haina kinga.'

Vilevile, wafanyakazi wa vituo vya mafuta wanapaswa kwa kiasi kikubwa kuzingatia usalama wa abiria kwa kukataa kuwajazia mafuta madereva wanaofuika kupata huduma hiyo, wakitambua wana mchango kwa usalama wa abiria.

Sheria za usalama barabarani, zinaainisha kuwapo makosa kwa gari la abiria kujaza mafuta huku abiria wakiwa ndani na endapo mtu anatiwa hatiani, kuna adhabu mahsusi iwe ya fedha au adhabu nyinginezo.

Pia anaongeza kuwapo kosa la kila mara, kwamba njia pekee ya kuepuka adhabu hizo, ni wahusika kutii sheria badala ya kulazimisha kufanya makosa.

Ni vyema sasa madereva na wasaidizi wao kutofanya kazi kwa mazoea kutokana na ukweli kwamba, imekuwa kawaida yao kujaza mafuta wakiwa na abiria, jambo ambalo mamlaka husika zimepiga marufuku.


Madereva hasa wa daladala hubeba abiria kupita kiasi, kwao ikiwa jambo la kawaida na wakati huohuo, kinga ya abiria dhidi ya mlipuko wa moto kwenye vituo vya mafuta ni madereva na wasaidizi wao wakitii sheria.

Wamiliki wa daladala ni wadau wa usafiri, hivyo wawasimamie vyema madereva na makondakta ili wazingatia kanuni na sheria za usalama barabani na ubora wa huduma pamoja na masharti mengine ya usafirishaji.

MAKALA MAALUM

# Buriani Maalim, mbuyu wa siasa za kihistoria Zanzibar umeng'oka

**Na Sabato Kasika**



Maalim Seif Sharif Hamad siku alipoapishwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (kushoto), kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. **PICHA: MAKTABA**

SERIKALI ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUK) imepata pigo kufuatia kifo cha Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, kilichotokea jana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam.

Kifo cha mwanasiasa huyo kilitangazwa kwa umma na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ikiambatana na siku saba za maombolezo ya msiba huo mzito, bendera kupeperushwa nusu mlingoti.

Maalim Seif ni mwanasiasa mwenye historia ndefu katika siasa za Zanzibar na Tanzania, mzizi wake ni tangu zama za mpito kutoka ASP kuelekea muungano wake na TANU kuiunda CCM, mwaka 1977.

Lakini, kwa kurejea mzizi wake katika mfumo wa utumishi wa umma, ambao pia ulikuwa chanda na pete na siasa za Zanzibar, Maalim Seif mzizi wake katika utumishi wa serikali visiwani, unarejea mwaka 1975.

Wakati huo akiwa kijana 'mbichi' mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ndio kipindi alipoingia katika utumishi wa umma, pale alipoteuliwa kuwa Msaidizi Binafsi wa Rais wa Zanzibar, Mzee Aboud Jumbe na hadi kufika mwaka 1977 aliteuliwa kuwa Waziri wa Elimu na Zanzibar hadi mwaka 1980.

Kisha alirejea katika chama CCM, alikoteuliwa kuwa Mkuu wa Uchuki na Mipango kwa upande wa Zanzibar hadi kufika Februari 1984, alipokwea tena kiserikali, akiteuliwa kuwa Waziri Kiongozi wa SMZ.

Ni kipindi ambacho siasa za visiwani zilikabiliwa na sintofahamu za ndani ya siasa, Maalim Seif akiwa mhimili ulioiva.

Alishikilia nafasi hiyo katika kipindi chote cha uongozi wa Rais wa Zanzibar wakati huo, Ali Hassan Mwinyi na mwaka 1985 alipochaguliwa Rais Idris Abdul Wakil (marehemu) kuongoza Zanzibar, bado Maalim Seif aliendelea katika nafasi hiyo hadi Januari, 1988.

Hapo kukashuhudiwa msuguano ambao unaobaki historia hadi sasa Zanzibar, hata ikaangukia kuondolewa kwake katika uongozi SMZ, sambamba na chama chake CCM, akishaitumikia serikali hiyo kwa nafasi ya juu miaka 12.

Mwanasiasa huyo, mtaalum wa sayansi ya siasa, elimu aliyoipata kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hakuipa kisogo siasa, bali alijitokeza katika sura mpya, baada ya kufukuzwa kutoka CCM, kutokana na kushindana na msimamo wa chama chake, kwa mambo kadhaa.

Ukawa ni wakati ulioshuhudiwa nguvu zake kisiasa, akiwa na wafuasi wake, hata kuna wakati ilishuhudiwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, alipofanya ziara maalum Zanzibar kuweka mambo sawa, ikiwamo ufafanuzi wa kufukuzwa Maalim Seif na baadhi ya wenzake.

Ni katika zama hizo joto la siasa za Zanzibar limepanda, kiatu chake cha uwaziri kiongozi kilirithiwa na mteule, Dk. Omar Ali Juma, wote wawili wakiwa na asili ya Pemba.

**RASMI UPINZANI**

Baadaye na wenzake wakiwamo Soud Yussuf, Mzee Mloo na Ali Haji Pandu, walikuwa waanzilishi wa vuguvugu Zanzibar lililoitwa "Kamahuru" iliyoungana na Chama Cha Wananchi (CCW), kuunda Chama cha Wananchi (CUF). Hapo, yeye akachaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa kwanza wa chama hicho hadi mwaka 1999 alipochaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa CUF.

Tangu uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1995 alikuwa akiwania nafasi ya urais wa Zanzibar kupitia chama hicho cha CUF kila uchaguzi, lakini alishindwa.

Katika harakati hizo za kwanza, Maalim Seif anatajwa kuwa ndio chanzo cha kumchukua rafiki yake wa chuo kikuu, Prof. Ibrahim Lipumba, kuwania urais wa Jamhuri ya Muungano naye akaweka kando chaki na kudumu katika siasa, hadi akipanda kuwa Mwenyekiti wa CUF Taifa.

Kuna wakati, uongozi wa Maalim Seif, Baraza Kuu la Uongozi CUF Taifa, lilimtimvua uanachama, mwanachama wake Hamad Rashid pamoja na baadhi ya wanachama.

Ilikuwa ni mwaka 2012 alipovuliwa uanachama, huku mojawapo ya sababu ya kukumbwa na tukio hilo ikiwa ni kukiuka katiba ya chama ambayo imeundwa na ndiyo inayowaunganisha wana CUF wote.

Hatua hiyo ilisababisha Hamad kujiunga na Chama cha ADC, kilichomwezesha kupata ujumbe wa Baraza la Wawakilishi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na hatimaye kuteuliwa kuwa Waziri wa Afya kwenye SMZ.

Mwaka 2016, uliibuka mgogoro wa kiuongozi ndani ya CUF kati yake na Prof. Ibrahim Lipumba na mwaka 2019 aliamua kujiunga na Chama cha ACT- Wazalendo na kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa taifa.

Maalim Seif Sharif Hamad alihudumu ndani ya CUF kwa kipindi cha miaka 26, baada ya Mahakama Kuu jijini Dar es Salaam kumthibitisha Prof. Ibrahim Lipumba kuwa mwenyekiti halali akaamua kuhama chama hicho.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana, Maalim Seif aliwania tena urais kupitia ACT- Wazalendo na kuwezesha chama hicho kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), ambayo hata CUF iliwahi kuwamo.

Itikadi yake, iliangukia falsafa aliyoiita 'haki sawa kwa wote' na alihimiza hilo katika siku zote za uhai wake, kwa lengo la kuwataka watu kutobaguana kwa itikadi za kisiasa.

Maalim Seif alizaliwa katika kijiji cha Mtambwe Nyali, kisiwani Pemba, Oktoba 22, mwaka 1943, alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Uondwe, 1950 na baadaye alijiunga na elimu ya sekondari katika shule ya watoto wa kiume Wete Pemba 1952.

Baadaye aliendelea na elimu ya sekondari katika Shule ya King George na kuhitimu kidato cha sita mwaka 1963, ambapo baadaye kati ya mwaka 1972 na 1975 alihitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kutunukiwa shahada ya kwanza ya Sayansi ya Siasa.

Kati ya mwaka 1972 na 1975 alifundisha katika shule mbalimbali za Unguja na Pemba, zikiwamo Fidel Castro na Lumumba. Alimuoa Fourtuna Saleh Mbamba na kuzaa naye mtoto mmoja na kisha akafunga ndoa na Aweina Sinani Masoud tangu mwaka 1977 na wana watoto watatu wote wa kike.

# Mabula ataka kitega uchumi Mutukula kukamilika kwa muda

**Na Munir Shemweta,** MISENYI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kukamilisha haraka mradi wa jengo lake la kitega uchumi lililoko Mutukula, Misenyi mkoani Kagera.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo jana akiwa katika ziara ya siku moja katika mkoa wa Kagera kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na miradi inayojengwa na NHC.

Alisema kukamilika mapema kwa jengo la kitega uchumi katika eneo la Mutukula siyo tu litaliwezesha shirika kupata fedha lakini litakuwa kichocheo cha wafanyabiashara wa Tanzania na Uganda.

"Mradi huu uko kimkakati ukikamilika tutapata wawekezaji na kasi ya wafanyabiashara kukimbilia upande wa pili itapungua, hivyo nataka jengo hili liishe kufikia Machi, mwaka huu," alisema.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, ujenzi wa mradi huo umechukua muda mrefu na kusisitiza kuwa kutokana na maendeleo mazuri ya ujenzi ni matumaini yake mradi huo sasa utakamilika kwa wakati.

Alisema mradi huo ni njia ya NHC kujenga majengo maengine ya biashara katika maeneo mengine na kuongeza kuwa miradi kama hiyo italisaidia shirika kimapato. Meneja Huduma kwa Jamii wa NHC, Muungano Saguya, alisema shirika lina mkakati wa kujenga majengo ya kibiashara katika maeneo ya mipakani ili kuimarisha biashara katika maeneo hayo.

Alisema pamoja na NHC kuendelea na ujenzi wa mradi wake katika eneo la Mutukula, liko katika mkakati wa kujenga vitegauchumi vingime katika meneo yote ya mipaka ya Tanzania na nchi zingine na kipaumbele kikiwa ni mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Sirari na Tanzania na Zambia, eneo la Tunduma.

Msimamizi wa mradi wa kitega uchumi cha Mutukula, Mhandisi George Shanali, alimweleza Naibu Waziri kuwa mradi wa jengo hilo unaendelea vizuri na unatarajiwa kukamilika Machi 15, mwaka huu.

Alisema mradi huo unaogharimu takriban Sh. bilioni 2.9 na utajumuisha huduma za kibenki na maduka 36 ya biashara.




Ofisa Masoko wa Benki ya TPB, Doroth Joseph (kushoto), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali vikiwemo vyakula kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Temboni, Patrick Kahwa, kwa ajili ya wanafunzi wenye Mahitaji Maalum shuleni hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Uwekezaji, utumiaji tiba asili wahimizwa

**Na Christina Mwakangale**

WITO umetolewa kwa Watanzania kuwekeza, kutumia na kuendeleza tiba asili, ili kukuza kipato chao na taifa.

Mtaalamu wa Mimea kutoka Shirika la Dawa Asili na Ulinzi wa Mazingira (TRAMEPRO), Dk. Isaac Mitoh, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe jana, kuhusu mchango wa tiba asili kwa jamii.

Alisema sekta mbalimbali hususan zilizojikita pamoja na wadau katika kuendeleza tiba hiyo, wafanye utafiti kutambua aina ya mimea inayotoa tiba kwa magonjwa na kurasimisha.

"Utafiti wa mimea na wanyama ambao, kwa ajili ya tiba asili inayoweza kusaidia katika magonjwa ikagundulika inasaidia na kupitishwa na mamlaka, itasaidia kuimarisha biashara nchini hata nje," alisema Dk. Mitoh na kuongeza:

"Tiba asili inahusisha maarifa, mimea kama taifa tukiweza kuendeleza katika uzalishaji wa dawa hizo na kuzifungasha kisasa, utaifanya Tanzania kuingia katika soko la dunia ambalo linahitaji tiba hiyo kwa kiwango kkubwa hivi sasa."

Alisema Tanzania inaweza kuingia katika soko la dunia kutokana na kukua kwa mahitaji ya tiba asili, na kwamba hadi kufikia mwaka 2026 uuzaji wa dawa za asili duniani utakuwa na thamani ya dola za Marekani 411.

"Tiba asili si kitu cha uchawi. Wizara inaweza kutusaidia kusimamia na kutoa mwongozo namna ya kuwapo mashamba maalumu ya mimea," alisema Dk. Mitoh.

Aliongeza kwamba wakati dunia ikiendelea kufanya utafiti wa tiba za magonjwa yasiyoambukiza, ni fursa kwa Tanzania kugundua ufanisi wa mimea inayotibu magonjwa.

# Walengwa TASAF wapanda miti kutengeneza madawati

**Na Marco Maduhu, KAHAMA**

WALENGWA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) walioko Bukondamoyo, Manispaa ya Kahama, wamepanda miti katika Shule ya Msingi Bukondamoyo, ili baadaye itumike kutengeneza madawati na kutatua tatizo la uhaba wa samani shuleni hapo.

Mwenyekiti wa kikundi cha wanawake 15 ambao ni walengwa wa TASAF walioamua kuanzisha mradi huo, Maria Bundala, alisema juzi kuwa baada ya kupata fedha za ruzuku kutoka mfuko huo, waliamua kuanzisha mradi huo wa upandaji miti kwenye eneo la ekari nane.

Alisema mradi huo waliuanzisha mwaka 2018 na kwamba mbali na kutatua tatizo la uhaba wa madawati, mbao hizo pia zitatumika kuezeka vyumba vya madarasa na miti hiyo ikivunwa, watapata kipato na kujikwamua kiuchumi.

"Tuliibua mradi huu wa upandaji miti katika Shule hii ya Msingi Bukondamoyo baada ya kuona uwapo wa tatizo la mmomonyoko wa ardhi.

"Tukapanda miti hii ya mbao ambayo itamaliza tatizo la uharibifu wa mazingira na mbao tutakazokuwa tukivuna, zitatumika pia kwenye utengenezaji wa madawati.

"Na sisi walengwa wa TASAF mradi huu utakuwa na faida kwetu. Mbali na kutatua changamoto ya madawati katika shule hii na ujenzi wa vyumba vya madarasa, tutakuwa pia tukiuza mbao kwa wafanyabiashara na kujipatia kipato na kuinuka kiuchumi," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Makaka Kizozo, alisema mradi huo wa upandaji wa miti ya mbao shuleni hapo umekuwa msaada mkubwa, akibainisha kuwa tatizo la mmomonyoko wa ardhi sasa limepungua, hasa kwenye maeneo ambayo miti ipo.

Alisema miti hiyo ya mbao itakapokuwa ikivunwa, itawasaidia pia kwenye utengenezaji wa madawati, akibainisha kuwa kwa sasa wana upungufu wa madawati 400.

Mwalimu huyo pia alisema shule hiyo kwa sasa inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 43.

HABARI KITAIFA

## NMB yawapa faraja wajawazito Kishapu

**Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB kupitia tawi lake la Kishapu imetoa msaada wa vitanda saba vikiwamo vitatu vya kujifungulia na mashuka 25 kwa hospitali ya Jakaya Kikwete ya halmashauri hiyo.

Msaada huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 5 unaotarajiwa kuoboresha huduma kwa wajawazito wilayani humo ulikabidhiwa na Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse.

Akikabidhi msaada huo ambao ni muendelezo wa misaada inayotolewa na benki hiyo kuboresha sekta ya afya na elimu sehemu mbalimbali nchini, Magesse alisema huo ni utekelezaji wa sera ya benki ya kurejesha sehemu ya faida kwa jamii.

Alisema benki hiyo imetenga bajeti ya Sh. bilioni 1 kwa mwaka kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na misaada wakati wa majanga ya asili.

"Pamoja na sekta ya elimu na afya, NMB pia hushirikiana na Serikali na wadau wengine kusaidia jamii wakati wa majanga ya asili. Haya ni maeneo matatu tunayoyapa kipaumbele katika miradi yetu ya kusaidia jamii," alisema Magesse.

Alisema benki hiyo imejikita katika miradi ya afya na elimu, kwa sababu sekta hizo ni maeneo muhimu kwa maendeleo na ujenzi wa Taifa.

"Ili kuendelea na kufanikiwa kiuchumi, Taifa linahitaji watu wenye afya njema na elimu bora; hii ndiyo maana NMB inasaidia maendeleo katika sekta za elimu na afya," alisema Magesse.

Mganga mkuu wa Halmashauri ya Kishapu, Dk. Shani Mudamu, alisema kupatikana kwa vitanda vitatu vya kujifungulia kutaiwezesha hospitali hiyo kuwahudumia wajawazito sita kwa wakati mmoja.

"Awali tulikuwa na uwezo wa kuwahudumia wajawazito wanne pekee kwa wakati mmoja. Sasa tutaweza kuhudumia sita huku kitanda kimoja kikiwekwa akiba kwa ajili ya dharura," alisema Dk. Mudamu. Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba, aliushukuru uongozi wa NMB kwa kuendelea kuchangia miradi ya maendeleo wilayani humo.

"Mwanzoni tulipokea Sh. milioni tano kusaidia kupaua vyumba vya madarasa na majengo ya zahanati; tukapokea Sh.milioni tano nyingine ilichochea wazo la ujenzi kujenga shule ya sekondari ya wasichana Kishapu, na leo tumepokea vitanda na mashuka vyenye thamani ya Sh. milioni tano. Tunaomba ushirikiano huu uendelee," alisema Taraba

# Mawakala wa forodha mipakani waonywa magendo

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imewataka mawakala wa forodha waliopo maeneo ya mipakani kutojihusisha na biashara za magendo, bali wafuate sheria na taratibu za forodha za kuingiza na kutoa mizigo nchini.

Agizo hilo lilitolewa na Ofisa Mkuu Utafiti, Sera na Mipango wa TRA, Happyson Nkya, alipokuwa akizungumza na mawakala wa forodha wanaofanya shughuli katika mpaka wa Sirari uliopo Wilaya ya Tarime mkoani Mara.

Nkya alisema mawakala ni kiungo muhimu kati ya TRA na walipakodi, hivyo wanapaswa kutoa taarifa sahihi kwa wateja wao kuhusu taratibu na kanuni za kutumia mpaka rasmi, ili kuwasaidia kutojihusisha na biashara za magendo ambazo zinaweza kuwaingiza katika hasara ya kufilisiwa mali. Nkya alisema: "Ninyi mawakala wa forodha mpakani ni kiungo muhimu sana kwetu na walipa kodi, hivyo tunawaomba msiwe mawakala wa biashara za magendo hapa mpakani bali muwe mabalozi wa kuwaelekeza wateja wenu taratibu za kiforodha ili serikali ipate mapato."

Mawakala wa forodha katika mpaka wa Sirari walifurahishwa na hatua ya TRA kufanya mazungumzo nao, kwamba wapo tayari kuwa mabalozi kwa sababu biashara za magendo zinaathiri pia biashara zao.

Mmoja wa mawakala hao kutoka Kampuni ya Sunrise Logistics, John Duro, alisema: "Sisi tupo tayari kuwa mabalozi na kuwaelekeza wateja wenu taratibu za kiforodha, kwa sababu wakipita kwenye mpaka rasmi ndipo na sisi tunafanya biashara zetu vizuri na serikali inapata mapato."

Wakala mwingine, Sncoslaus Nyang'oko, kutoka Kampuni ya E3, alisema suala la biashara ya magendo mpakani limekuwa likidhorotesha shughuli zao, hivyo watashirikiana na serikali katika kuhakikisha kuwa magendo yanakuwa siyo sehemu ya biashara zao na kuwaelekeza wateja wao kutumia mpaka rasmi wa Sirari. "Mawakala wa forodha tunafanya shughuli zetu kwa mujibu wa taratibu na kanuni za kiforodha, hivyo hatuwezi kuwa sehemu ya kufanya biashara haramu za magendo, tunakubali kuwa mabalozi wa kuwaelekeza wateja wetu kutumia mpaka rasmi," alisema Nyang'oko.

TRA imekuwa ikifanya mikutano na wadau mbalimbali mkoani Mara ili kutoa elimu kuhusu taratibu za kiforodha za kufuata wakati wa kuingiza na kutoa mizigo katika mpaka wa Sirari. Lengo la mikutano hiyo ni kujenga uelewa wa matumizi ya mpaka rasmi na kukabiliana na biashara za magendo mpakani hapo.




Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba (wapili kushoto), akipokea moja ya vitanda kutoka kwa Meneja wa Kanda ya Magharibi wa NMB, Sospeter Magesse, ambapo benki hiyo ilikabidhi pia vitanda vitatu vya kujifungulia na vinne vya kawaida na magodoro yake, pamoja na mashuka 25 kwa ajili ya Hospitali ya Jakaya Kikwete. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhaba wa walimu kikwazo kwa Masasi

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, inahitaji jumla ya walimu 955 wa shule za msingi ili kuongeza ufanisi na kuinua kiwango cha ufaulu katika sekta ya elimu.

Hayo yalisemwa jana mjini Masasi na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Changwa Mkwazu, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusu changamoto mbalimbali za elimu kwa halmashauri hiyo.

Alisema halmashauri ina jumla ya shule za msingi 131 na vyumba vya madarasa vilivyopo ni 764, ila changamoto kubwa katika hasa katika elimu msingi ni uhaba wa walimu.

Alisema kwa sasa mahitaji ya walimu kwa shule za msingi ni 955, huku waliopo ni 910 na kwamba upungufu wa walimu katika halmashauri hiyo ni 711na mahitaji halisi ni 955, hivyo ikiondokana na changamoto hiyo, itafanikiwa kuwa juu kitaaluma miaka ijayo.

Mkwazu alisema hali hiyo inapelekea halmashauri kuwa na changamoto ya walimu ambapo ni moja ya kikwazo cha maendeleo ya elimu kwa halmashauri hiyo.

Alisema kuwa halmashauri hiyo imekuwa katika nafasi ya nane kati ya halmashauri tisa za Mkoa wa Mtwara kwa mwaka 2020 nafasi ambayo sio ya kuridhisha ukilinganisha na miaka ya nyuma.

"Tunaiomba serikali iendelee kutuangalia kwa kutupatia walimu wa kutosha ili kuondoa upungufu wa walimu waliopo hatimaye tuweze kuongeza hali ya ufaulu katika sekta ya elimu Masasi," alisema Mkwazu.

Alisema iwapo kila shule ikiwa na walimu wa kutosha hata ufundishaji utafanyika kwa ufanisi zaidi kwa sababu ikama ya walimu inatosheleza.

Naye Ofisa elimu msingi wa halmashauri hiyo, Elizabeth Mlaponi, alisema changamoto kubwa inayosababisha kuwapo kwa mahitaji makubwa ya walimu katika idara ya elimu msingi kwa halmashauri hiyo ni idadi kubwa ya walimu kustaafu pamoja na vifo.

Alisema licha ya upungufu wa walimu uliopo kuna kila sababu kwa walimu wanaofanya kazi katika halmashauri hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kujituma ili kutimiza malengo ya kuinua kiwango cha taaluma kwa halmashauri hiyo.

"Kiwango cha ufaulu kimepungua kwa asilimia 1.17 kutoka asilimia 64.87 kwa 2019 hadi kufikia asilimia 63.7 kwa mwaka 2020, hivyo wazazi, walimu na jamii kwa ujumla tunapaswa kushirikiana katika sekta ya elimu ili kuongeza thamani ya taaluma," alisema Mlaponi.

# Walalamikia mradi wa chumvi hifadhini

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa uchimbaji chumvi unaofanywa katika kijiji cha Buyuni, Kata ya Mkwaja, Wilaya ya Pangani, Mkoani Tanga, umedaiwa kutishia maisha ya wanyamapori waliopo katika Hifadhi ya Taifa ya Saadani.

Kijiji cha Buyuni kinapakana na Hifadhi hiyo ambapo kimetoa hekari zaidi ya 20 kwa mwekezaji, Nasil Salehe, kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya chumvi katika eneo hilo.

Baadhi ya majirani na mradi huo wamezungumza na waandishi wa habari waliotembelea mradi huo na kujionea uharibifu wa mazingira ikiwamo ukataji wa mikoko inayozunguka Bahari ya Hindi na uchimbaji mitaro ya maji jambo linalohatarisha makazi ya wanyama. Akizungumza kwa niaba ya majirani wenzake Mpalangwe Ansyle, alisema wameshangazwa na uongozi wa kijiji hicho kutoa eneo hilo kwa ajili ya uchimbaji madini huku wakitambua kuwa ni makazi ya wanyamapori.

"Kijiji hiki kipo jirani kabisa na hifadhi hii, tena kuna wakati wanyamapori wanaofika hadi ndani ya kijiji tumeshangaa kuona uongozi ukigawa eneo ambalo hata wanyamapori wamekuwa wakiishi hapo," alidai.

Alidai uchimbaji uliofanywa katika eneo hilo kama hatua za haraka hazitachukuliwa zinaweza kusababisha athari za kimazingira na hata kupoteza baadhi ya wanyamapori kwa kuwa wakitumbukia katika mabwawa haya watapoteza maisha.

Waliziomba mamlaka husika hasa za kitaifa kufuatilia mradi huo ili kujiridhisha kutokana na kuwapo kwa ukataji ovyo wa mikoko ya bahari pamoja na uharibifu wa kimazingira.

Ofisa Mazingira Wilaya ya Pangani, Daudi Mlahagwa, alisema, anaufahamu mradi huo, lakini hawezi kuuzungumzia bali atafutwe Mkurugenzi wa Wilaya hiyo ili aweze kufafanua zaidi.

Alipotafutwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Isaya Mbenje, alisema, mwekezaji huyo alifuata taratibu zote za kuwekeza katika eneo hilo na kuongeza kuwa amekuwa akilipa kodi kwa wakati.

Hata hivyo, alisema katika eneo hilo kuna mikoko ambayo inaendelea kukua vizuri kwa ajili ya utunzaji wa mazingira hasa kutokana na maelekezo yanayotolewa na maofisa wa mazingira juu ya eneo hilo.

Kuhusu wanyama kukimbia, alisema hawawezi kuwekewa mipaka ni mahali gani wanatakiwa kufika na wapi wasifike, hivyo mara nyingi hufikia hadi kwenye eneo la mwekezaji huyo na katika makazi ya wananchi wa kijiji hicho.

Aidha, alisema, kwa kuwa kijiji cha Buyuni chenye wakazi wapatao 280 kimezungukwa na hifadhi, ameitaka TANAPA kuangalia ni kwa namna gani wataweza kuwahamisha wananchi kwa kuwapatia eneo jingine.

"Hichi kijiji cha Buyuni chote kimezungukwa na hifadhi, wananchi wanaoishi maisha yao yapo hatarini, maana wanyama huvamia katika makazi yao, kuna kipindi wananchi wanalazimika kulala saa 12 jioni au wasitoke ndani kutokana na wanyama wakali kufika katika eneo hilo... sisi kama serikali tunafanyia kazi ili kuhakikisha jamii iliyopo pale iweze kuishi vizuri."

"Haya ni mambo ambayo kwa kushirikiana na TANAPA tutaangalia ni kwa jinsi gani tunaweza kuwawezesha wananchi hasa kwa kuwatafutia eneo jingine la kuishi ili shughuli za hifadhi ziweze kuendelea," alisema.

Alipotafutwa pia Kaimu Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Saadani, Prisca Lyimo, alisema, kwa sasa hayupo tayari kuzungumzia mradi wa mwekezaji huyo kwa sababu anatakiwa kupeleka taarifa makao makuu juu ya kinachoendelea katika eneo hilo.

"Natakiwa kupeleka taarifa makao makuu juu ya mradi huu hivyo siwezi kuuzungumzia kwenye vyombo vya habari mpaka pale nitakapokamilisha taarifa yangu," alisema.

Mwenyekiti wa kijiji cha Buyuni, Diwani Waziri, alisema mradi huo wa uchimbaji chumvi unaomilikiwa na Nasa Salehe ulioanza 2016 umekuwa msaada mkubwa kwao.

Alisema mwekezaji huyo amekuwa akiwasaidia katika huduma mbalimbali za jamii ikiwamo kuwachimbia mabwawa ya kupokea maji ya mvua.

"Chini ya ardhi yetu kila ukichimba kutafuta maji utakutana na maji ya chumvi, lakini mwekezaji huyu amefanikisha kupatikana kwa maji baridi na ujenzi wa mabwawa ya kupokea maji ya mvua," alisema.

Kuhusu wanyama, alisema wamekuwa wakifika katika eneo hilo la mwekezaji, lakini ameutupia lawama uongozi wa TANAPA kutokana na kushindwa kuwasaidia wananchi wanaokaa katika kijiji hicho.

"Tangu kijiji kianzishwe au wazee wetu wakae hapa mpaka sasa hatuna zahanati ila mwekezaji ameshaanza mchakazo wa kutujengea, hivyo sisi tumempa ardhi na tumeona kwa kipindi kifupi tu amekuwa msaada kwetu," alisema.

Kwa upande wake, mwekezaji huyo alisema amefuata taratibu zote za kupata eneo hilo, huku akiwa na vibali vyote vikiwamo vya madini, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kwamba analipa kodi zote katika Halmashauri hiyo.

"Nimefuata taratibu zote katika kupewa eneo hili na kama ulivyoshuhudia, huu ni uwekezaji mkubwa tunafanya utatoa ajira nyingi utakapoanza," alisema.

Kuhusu suala la wanyamapori kutoweka katika eneo hilo, Salehe alisema hiyo haiwezi kuwa sababu ya kuzuia kufanyika kwa mradi huo kwa kuwa eneo hilo ni la kijiji lakini lipo jirani na hifadhi hiyo.

Alisema kuwa mradi huo ni rafiki wa mazingira, hivyo anashangazwa na wanaoulalamikia.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa darasa la awali katika Shule ya Msingi Busamba, kitongoji cha Egenge, Kijiji cha Busamba, Kata ya Etaro, Musoma Vijijini mkoani Mara juzi, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya serikali ya kutaka kila shule ya msingi kuwa na madarasa hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenyeviti, watendaji watakiwa kushirikiana

**Na Yasmine Protace,**

MKURANGA

WENYEVITI wa vijiji na watendaji wao, wametakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuwaondolea wananchi vikwazo vinavyowakabili katika maeneo yao.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mkuranga, Mhandisi Mushamu, katika kikao kazi kilichofanyika wilayani hapo.

"Wenyeviti wa vijiji na watendaji, mnatakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuwatatulia wananchi vikwazo katika maeneo yakiyowazunguka," alisema.

Aliongeza kuwa wataalamu wanatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria za taratibu na mwongozo kuhakikisha utekeleza wa ilani ya CCM unazingatiwa.

Munde alisema kupitia mwongozo wao wa TAMISEMI Halmashauri hiyo inayotegemea kukusanya na kutumia mapato ya ndani Sh. bilioni 7.8 mwaka wa fedha 2022/23 inatatarajia kujenga kituo cha afya na vyumba 40 vya madarasa.

Aliwataka watendaji na wataalamu kufanya kazi kwa kuzingatia uadilifu, huku akisisitiza kuanzia sasa suala la uhamisho kwa atakayevurunda kituo cha kazi halipo bali taratibu za kinidhamu zitachukuliwa.


**"Wenyeviti wa vijiji na watendaji, mnatakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuwatatulia wananchi vikwazo katika maeneo yakiyowazunguka," alisema.**

ama
ALHAMISI FEBRUARI 18, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**MAJANGA AFYA ZIWANI VICTORIA**




Ukurasa 14

**DK. CHIDUO-TANGA:**

**NIMR mbioni kutoa majibu chanjo ya malaria kimataifa**

# Korea Kaskazini yashutumiwa kuiba taarifa za utengenezaji chanjo corona

## •Bosi mpya WTO ana lake la mada hiyo

SHIRIKA la ujasusi la Korea Kusini limeshutumu Korea Kaskazini, kwa madai ya kuvamia kampuni ya Pfizer, ikijaribu kuiba teknolojia inayotumika kutengeneza chanjo ya virusi vya corona.


Madai kutoka kwa maofisa wa kijasusi wa Korea Kusini, ni kwamba ilikuwa mbinu ya kuchukua teknolojia inayotumika kutengeneza chanjo ya virusi vya corona kutoka kampuni ya utengenezaji dawa ya Marekani Pfize.

Hata hivyo, haijawa bayana namna gani ya taarifa zilizoibwa, huku kunaripotiwa kuwa Shirika la Kijasusi la Korea Kusini, limeamua kuchukua hatua binafsi ya kuwataarifu wabunge juu ya kinachodaiwa kuwa 'uvamizi.'

Hadi sasa kampuni ya Pfizer inayolalamika haijatoa tamko lake na wakati huohuo, Korea Kaskazini nayo haijawahi kuripoti chochote kuhusiana na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona katika eneo lake.

Korea Kaskazini iliyofunga mipaka yake mnamo mwezi Januari mwaka jana muda mfupi baada ya ugonjwa wa virusi vya corona kuanza kujitokeza nchini China, inaelezwa ndani ya muda mfupi, wiki chache zijazo inatarajiwa kupokea dozi milioni mbili za chanjo ya AstraZeneca.

Mnamo mwezi Novemba iliyopita, kampuni ya kimataifa ya



Mkuu mpya wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala. **PICHA: MTANDAO.**

Microsoft, ilisema takriban mashirika tisa, ikiwamo Pfizer, zililengwa na mashirika yanayoungwa mkono na serikali nchini Kore Kaskazini na Russia.

Inasemekana kuwa makundi ya mashirika ya Korea Kaskazini na kundi linalojulikana kwa jina la utani 'Fancy Bear' kutoka Russia, yalihusika katika uvamizi huo.

Pia, kunadaiwa utafiti wa chanjo nyinginezo ulifeli, huku kampuni ya Microsoft ikisema kuna sura ya mafanikio

**UCHAMBUZI WA USALAMA**

Gordon Corera, mwanahabari aliyejikita katika masuala ya usalama, anasema kutoka zama za janga la virusi vya corona, mataifa yamekuwa yakiweka wavamizi wake kama sehemu ya janga la virusi la corona.

Baadhi ya wavamizi wamekuwa wakikusanya taarifa za kijasusi na baadhi wanatekeleza wizi wa haki za uvumbuzi.

Kunadaiwa kuwapo uwezekano, Korea Kaskazini imekuwa moja ya nchi iliyo mbioni kupata taarifa nyeti, huku ikiwa ni jamii iliyojifungia.

Ni kati ya mataifa yanayoonekana kuwa na ujuzi wa hali ya juu wa masuala ya mtandaoni na imekuwa tayari kulenga nchi nyinginezo kupata siri zilizohifadhiwa, kwa malengo mbalimbali.

Mwaka jana nchini Uingereza, Kituo cha Usalama wa Mtandao wa Kitaifa, kiliweka ulinzi mkali katika utafiti wake wa chanjo na mwaka huu, angalizo limeelekezwa katika usambaaji na utoaji wa chanjo hiyo.

Suala la ubuninfu wa chanjo mbalimbali duniani, ikiwamo wa corona imekuwa mada kuu katika sura nyingi, kila taifa ikiwa na mwelekeo wake wa kitafsiri na msimamo.

**KUTOKA WTO**

Mkuu mpya wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala, anasema ubunifu wa chanjo mpya duniani unapaswa kusaidia kutatua janga la maradhi na si vinginevyo.

"Dhana ambayo mataifa tajiri yanawachanja watu wao na nchi masikini zinapaswa kusubiri lazima iepukwe," anasema.

Hivi karibuni nchi kadhaa zimejaribu kuzuia usafirishaji wa chanjo nje ya mipaka yake, jambo ambalo bosi huyo wa WTO anasema, hakukuwa na manufaa chanya kuzuia adha ya kuenea maradhi hawa ya kuambukiza.

"Asili ya janga na kubadilika kwa maumbile yanayosababisa aina tofauti za virusi, kunafanya kwamba hakuna nchi inayoweza kujihisi iko salama, hadi pale kila nchi itakapochukua tahadhari kuwachanja watu wake," anafafanua.

Dk. Okonjo, hadi mwishoni mwa mwaka jana alikuwa Mwenyekiti wa Muungano wa Dunia wa Chanjo (GAVI), uliolenga kuongeza upatikanaji chanjo duniani kote na sasa anasema WHO ina wakati mgumu kulishughulikia hilo.

Kuna mjadala unaoendelea sasa duniani, kuhusu kulegea kwa sheria za WTO na haki milki za watengenezaji dawa. Anasema, baadhi ya nchi zinazoendelea zinahisi kuwa hiyo inaweza kuingilia kati haki miliki zao.

• ***Makala hii ni kwa mujibu wa BBC.***

AFYA

# MAJANGA AFYA ZIWANI VICTORIA

- Chumba kimoja, wakazi saba, mazingira...
- Mama 'vichanga' wenye tofauti mwaka
- Ana umri 22; mavazi yake na watoto shida
- Mwaloni, neno ngono halina kigeni
- DC Ilemela: Kuna visiwa vitatu hali ni balaa

**Na Neema Emmanuel,**

**MWANZA**

KWA maisha ya kawaida ya Watanzania, wengi wanaangukia kundi la utafutaji. Ushuhuda wa jamii ya namna hiyo, ndio undani wa simulizi ifuatavyo:

Ni wakazi wa chumba kimoja cha kupanga, ambako ndiko faragha yao kuanzia kujipumzisha, mapishi na stoo. Ni inayowanyima amani wakazi na hata wapatapo wageni.

Humo ndiko unawakuta wenyeji familia ya Busalu (jina lingine tunalo) wa umri miaka 45, mvuvi wa samaki katika mwalo wa Butuja wilayani Ilemela, kwenye familia ya watu saba. Kuna shida ya afya, inayoegemea uchumi,

Ni mahali penye safu inayoishi ndani ya chumba kimoja, wakiangukia kwenye karaha za kila aina. Pakoje? Mtu anapoingia tu, anakaribishwa na mazingira yasiyo rafiki na harufu kali.

Ndani humo kuna sauti kali ya mtoto mchanga wa kike mwenye umri mwezi mmoja duniani, akidai kuhitaji chakula kutoka kwa mama. Kando yake, kuna mama anayemnyonyesha mtoto katika mazingira yasiyo rafiki kwa namna nyingi.



Ndio maisha halisi yaliyoko mwaloni, Ilemela. **PICHA ZOTE: NEEMA EMMANUEL.**

Akizungumza na Nipashe, Busalu , mwajiriwa wa uvuvi anakiri ushuhuda huo ndio umebeba uhalisia wa maisha yake, anasema ugumu wa maisha hayo ndio yanaitesa familia yake, kipato hakiendani na mahitaji halisi.

Mvuvi huyo anataja anachoambulia kwa siku ni kati ya Sh 5,000 na panapo neema, Sh 15,000, akisema ni aina ya ugumu wa maisha inayoambatana na changamoto binafsi.

Anasema mwanawe wa nne kuzaliwa mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu, kwa sasa anasumbuliwa na maradhi selimundu (sickle cell), yanayomdhoofisha mwili wake, huku akiwa bado anapata lishe duni huku akiyumba kiafya.

Ni hali inayoangukia kila wakati mtoto anasumbuliwa na maradhi hadi kulazwa katika Hospitali ya Rufani Sekou Toure, jijini Mwanza na baadaye Hospitali ya Kanda Bugando, walikobaini anaumwa selimundu.

Busalu anayeapa dhamira kumsindikiza mkewe hospital akapatiwe huduma ya uzazi wa mpango, anadokeza uduni wa maisha yao kwamba:"Siku tukikosa inakuwa siri ya ndani. Kuna wakati naondoka naenda ziwani (Victoria) sijamuachia mke wangu chochote.

"Siku tukikosa kabisa tunamuachia Mungu, nanunua maandazi watoto wanakula na maji sisi tunakunywa maji tu tunalala. Mfano leo hadi sasa hivi ni saa nane (siku aliyoongea na Nipashe) sijajua tunakula nini, watoto hawajala chochote tangu asubuhi.

"Mke wangu ananyonyesha mtoto wangu ana mwezi mmoja tangu azaliwe na mfukoni nina elfu mbili tu naona hii itatumika kununua maandazi ili watoto wale usiku."

### MAMA NAYE

Mama huyo mwenye umri miaka 22 (majina tunayo), analalamika kuumwa mguu na anashindwa kunyanyuka, anawaleza watoto wake, hatima ya mlo unaofuata kwao na upatikanaji wake ulivyo fumbo; kula au kushinda njaa.

Anasema, amekuwa akikatisha huduma ya selimundu, kia mtoto anapofika umri wa mwaka mmoja na miezi sita na kwa mtoto mwenye tatizo la selimundu, huwa ana kawaida kwenda naye mara moja moja, akitarajia kwenda naye atakapompeleka mwenye mwezi mmoja .

Mama huyo anasema, hana utaratibu wa kujiweka katika usafi , akizungumza hayo wakati akimnyonyesha mtoto mchanga asiyekuwa na nguo mwilini tangu ajifungue, akidai hana nguo hivyo majirani walimstiri .

"Mavazi nikipata hela nanunua nikikosa basi, kwa sababu vazi siyo ugali ambao ukila unaisha, unaweza ukawa na nguo mbili ukavaa mwaka mzima, ukivua hili unafua unavaa nyingine.

"Kwa sasa nina hali ngumu, naumwa mguu na sina matumaini ya maisha. Nilipokuwa mjamzito nilikuwa nauza pombe ya kienyeji, lakini baada ya kujifungua fedha niliyokuwa nayo nikatumia kwa ajili ya uzazi kwa sasa sina chochote," anasema .



Masato Hamisi, mkazi jirani na familia hiyo iliyozungumza na Nipashe, anakiri ukweli wa magumu ya yanayosumbua, hata watoto wao kuwa na njia panda, ikiwamo ya kiafya.

Rai yake ni kwamba kutolewe elimu ya kutosha kuhusiana na uzazi wa mpango na itolewe kwa wingi,

kwani sehemu kubwa ya jamii iliyoko maeneo ya mialo, hawana uelewa sahihi wa jambo ukiukwaji mkubwa wa uzazi wa mpang katika maeneo hayo.

### VIONGOZI SERIKALI

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Dk. Severine Lalika,anaiambia Nipashe kuwa katika maeneo ya mialo ya samaki upasuaji mbao ,madini na masoko, kuna hatari inayotokana na kuhamiri starehe, ongezeko la watoto, hali duni ya maisha, mimba zisizotarajiwa na maradhi mbalimbali, ikiwamo UKIMWI.

Anasema, wataalamu afya wilayani kwake, wana ratiba ya kila mara wanahamasisha masuala ya afya na katika kata zote 19 hasa kwenye maeneo ya mialo, kwa sababu ndiko kuna yanayoenda kinyume na maadili, pia nyendo kitaifa.

"Hizo hali zinawapeleka watoto wetu wa kiume na kike, hata wale ambao wapo kwenye umri wa kwenda shule kupenda kujihusisha na shughuli za uvuvi. Wakiwa

huko wanakutana na adha mbalimbali, kwa kuwa hawajafikia umri wa kujitambua na kujikinga kiafya," anasema Dk. Lalika.

Mkuu wa Wilaya anasema, utoro wa watoto shuleni umeshamili hasa katika maeneo ya uvuvi, akitoa mfano wa baadhi wanaotelekeza shule na kuhamia mialoni katika ngazi za madarasa ya pili hadi la nne.

Sasa kiongozi huyo mkuu wa serikali wilayani, anawataka wakazi wa mwaloni kushirikiana na serikali, kuhakikisha watoto wenye umri wa kwenda shule hawashiriki kwenye ajira, kwani ni kukiuka sheria za nchi.

"Kuna visiwa vinaitwa Bezi, Igombe na Makobe. Huko ukienda kuna starehe ambazo ukiambiwa huwezi kuamini. Maeneo kama hayo yana madhara kiafya, hivyo wakazi waliopo katika maeneo ya mialo wametakiwa kuwa na mtazamo chanya wa elimu inayotolewa na maofisa afya," anaeleza Dk. Lalika.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Butuja, Kichonge Mwita, anachangia:"Tumetoa elimu ya uzazi kwa kushirikiana na wahudumu afya ngazi ya mtaa, tumewafikia wananchi wengi."

"Hivi karibuni tuliitisha mkutano wa hadhara kuwapa elimu na maelekezo, mwanzo hali ilikuwa ya hatari, lakini kwa sasa kidogo mambo yanaleta matumaini," anasema, huku akiomba mialo izingatie mafunzo wanayopewa kuwajenga wanafamilia.

Anadokeza uzoefu wea hatari kuna wakati baadhi ya wazazi wanawakimbia watoto wakiwaacha wanaranda mtaani.

### MTAALAMU AFYA

Mtaalamu Muwezeshaji wa Huduma za Afya ya Uzazi wa Kujitegemea Dk. George Lugodisha, anasema kukosekana taarifa sahihi na za kutosha kuhusu afya ya uzazi, ngono za mapema bila ya ufahamu sahihi wa kujikinga ni tatizo kubwa.

Anataja silaha yake ni mambo mtambuka, yanayojumuisha kutolewa taarifa sahihi za afya ya uzazi na athari za ukatili huo,akiwa na hitimisho:"Hakika afya ya uzazi imeweza kupunguza maambukizi ya magonjwa mbalimbali na kushamiri utoaji wa mimba mitaani."



Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Dk. Severine Lalika.

AFYA

## Mjue mkeketaji miaka 40, leo hataki hata kusikia neno hilo

- Mzazi, asiye na mtoto bei zao tofauti
- Wazee wa mila 'wakomba' Mapato
- Alihamia Dar akaendeleza kwa siri

**Na Yasmine Protace**

UKEKETAJI ni adha yenye madhara kwa jamii. Sehemu ya mambo yanayochangia ni kuwapatia makovu makubwa waliokeketwa na wengine kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua.

Haishii hapo, kwani inaelezwa kuwa hata wanafunzi wanaofanyiwa ukatili, wapo wengi wanapatwa na hasara ya kutofanya vizuri masomoni na wapo wanaohofu kucheza na wenzao, wakitawaliwa na nafsi ya woga.

Wahusika wakuu wa hayo yanayodaiwa kufanyika kwa siri ni kina nani? Nipashe ilibahatika kukutana na mkazi wa Tarime, Bhoke Mussa, anayedaiwa kudumu katika 'taaluma' hiyo kwa miaka 40 kabla ya kustaafu.

Mama huyo, leo hii anatamka kuwa kinyume na uhalisa aliyokuwa nao awali kwamba "anaichukia kazi hiyo baada ya kupatiwa elimu na kuelewa madhara yatokanayo na ukeketaji."

Bibi Bhoke ana simulizi kuhusu alikotoka kwamba kabla ya kuolewa katika ndoa iliyompatia mtoto pekee wa kike, alikeketwa.

Leo hii binti huyo sasa amempatia Bibi Bhoke, wajukuu watano walio katika mgawanyiko; mabinti watatu na wawili wakiwa wavulana, huku mzee huyo hajapata elimu yoyote maishani na hajui umri wake.

### SAFARI YA KUKEKETA

Anasema, ilikuwa mithili ya uteuzi kutoka kwa wazee wa kimila walimwambia 'ameonekana ana uwezo wa kukeketa watoto.'

"Nikiwa nyumbani, mume wangu akaniambia naitwa na wazee wa kimila. Nilienda kuwasikiliza na nikaambiwa mimi nafaa kukeketa watoto na kama nitakataa kufanya kazi hiyo, nitatumiwa," anasimulia.

Hapo ndipo anasema, alikubali na ndio ukawa mwanzo wa kuwajibika kwake na majukumu ya ukeketaji nyumbani Tarime, akifafanua kazi hiyo katika makazi ya watu.

Mwanzo wa kazi hiyo, alianza na kukeketa watoto watatu kwa siku akilipwa wa malipo wastani wa shilingi 30,000 kwa kila mtoto mmoja, lakini bei hiyo ilipanda kwa kinamama waliokwishajifunga, kufika Sh. 50,000.

Bibi Bhoke anasimulia kwamba kadri muda ulivyosonga, alipata uzoefu na hata akasonga kwa kukeketa kwa siku watoto 100.

Hata hivyo, analo la upande wa pili kwamba, hajanufaika na 'maelfu' aliyokuwa akiyaingiza, kwa sababu pesa nyingi zilichukuliwa na wazee wa kimila, binafsi akiambulia 'kiduchu.'



Bhoke Mussa, akiwa katika ujasiriamali wake jijini Dar e Salaam. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

### MAISHA MAPYA DAR

Bibi Bhoke anasema, baadaye alihamia jijini Dar es Salaam katika kitongoji nje ya jiji, akiendeleza kazi hiyo na kwa bei ilele na wateja wake ni wenye asili ya mahali alikotoka, wilayani Tarime.

Mama huyo anasema, wakati akiwa jijini Dar es Salaam, alipata habari naye yamemkuta ya 'muosha huoshwa'binti yake aliyemuacha Tarime alikeketwa,

Bhoke anasema wakati akiendelea na kazi, ndipo akapatiwa mafunzo yaliyotolewa na kituo cha taarifa na maarifa Kipunguni, Dar es Salaam na ndio ukawa mwisho wake kukeketa.

Mama huyo ambaye sasa ni mjasiriamali 'kindakindaki' anasimulia baada ya kupatiwa mafunzo, alipatiwa mbadala wa kujikimu kiuchumi; matuta nane na mbegu za mboga, ahamie katika kilimo.

Huo ndio ukawa mwanzo wa maisha mapya ya ujasiriamali na kulifanya jiji la Dar es Salaam, makazi yake ya kudumu, akiyaeleza mageuzi kwamba "Mafunzo yamenisaidia. Sasa sikeketi mtu na pesa naingiza kila siku ninapouza mboga."

Anasema kipato chake cha ujasiriamali mboga kinamsaidia kujikimu kimaisha, akiwa na imani mangaliba wote wakiwezeshwa kama yeye, wataacha kukeketa na kurejea maisha ya kawaida.

Bibi Bhoke 'anafunguka' kwamba kukeketwa kunamsababishia mwanamke kuovu la kudumu na hasikii hamu ya tendo la ndoa, mbali na madhara aliyojifunza

wanaokeketa na kukeketwa wote wapo katika hatatihati kupata magonjwa.

### WANA MAGEUZI

Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa, Kipunguni jijini Dar es Salaam, Selemsni Bishagazi, anasema katika mapambano yao dhidi ya ukeketaji, wamebaini dawa sahihi ni kuwaelimisha na kuwawezesha mangariba, inafanikisha kuwaachisha ukeketaji.

"Tukiwahoji ngariba wengi, wanakwambia wakiwezeshwa wataacha kufanya ukeketaji, kwa sababu wanafanya ukeketaji ili kujipatia kipato," anaeleza Mkurugenzi.

Anarejea mfano wa Bibi Bhoke, kwamba baada ya kugundua nyendo zake za kukeketa mara mbili kwa mwaka, waliamua kukampatia elimu na mtaji wa matuta ya kulima mboga, yanayomuingizia wastani wa Sh. 20,000 kila siku, kipato kikubwa kushinda cha msimu wa ukeketaji.

Bishagazi anasema wameanzisha klabu ya kupinga ukatili ndani ya jamii, lengo ni kuhamasisha ushiriki wa kuzuia vitendo hivyo, kwani takwimu zinaonyesha ukatili huanzia nyumbani na wafanyao ni wa karibu.

Anasema, katika klabu hiyo huwa wanakutana mara mbili kwa mwezi, wanakielimishana shubiri ya ukeketaji, ulawiti na ubakaji na jamii inalemishwa namna ya kutoa taarifa sahihi katika vita hivyo.

"Awali watu walikuwa wanafumbia macho matukio ya ukatili yanayofanywa na hatua zikawa hazichukuliwi. Baada ya elimu kutolewa, jamii imelimika na kutoa taarifa juuya matukio ya ulawiti,ubakaji,ukeketaji na ukatili wa aina mbalimbali," anasema.

Bhoke anasema mwanamke anayekeketwa akifikisha umri wa miaka 40, huwa anapoteza hisia kabisa ya kuhitaji tendo la ndoa.

Pia, anasema mama mara nyingi akiwa amekeketwa hatoki katika ndoa yake na kwa sababu anaona aibu uhalisi kujulikana kwingineko, hali inayowapa wanaume kutoka jamii za wakeketaji kung'ang'ang'ania tendo hilo batili.

AFYA

## DK. CHIDUO-TANGA:

# NIMR mbioni kutoa majibu chanjo ya malaria kimataifa

## •Taa ya kijani tafiti za Korogwe, Handeni

**Na Lulu George,TANGA**




Watoto katika kampeni zinazohusiana na kudhibiti malaria.

AFYA ya mama na mtoto, ni kipaumbele mahususi cha kuyafikia Malengo ya Milenia. Mwongozo wa serikali, ukishirikiana na wadau wa maendeleo kitaifa, kuhakikisha inapambana ugonjwa malaria.

Hapo kuna suala la utafutaji dawa na vifaa kinga kama vyandarua, vinavyoondoa usugu kwa mwanadamu yameshuhudiwa na kwa kiasi kikubwa yanapunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya wa miaka mitano.

Suala la kumsababisha mtoto upungufu wa damu, nalo linatajwa sana, huku serikali katika kutafuta suluhu ya kudhibiti ugonjwa, imegawa majukumu kwa asasi mbalimbali nchini.

Katika maadhimisho ya miaka 40, Kaimu Mkurugenzi wa kituo cha NIMR, Tanga Dk. Mercy Chiduo anasema wanajitahidi kutafuta kinga ya malaria, wakishirikiana na asasi nyinginezo za utafiti, kupitia majaribio ya chanjo kwa watoto wa umri chini ya miaka miwili, katika wilaya za Korogwe na Handeni.

Dk.Chiduo anasema, matokeo ya awali ya utafiti huo, yalionyesha mafanikio makubwa katika kupunguza vifo vitokanavyo na malaria na kupungua maambukizi ya kila mara kwa watoto waliopewa chanjo hiyo.

Anasema, ni utafiti huu wa chanjo iliyobatizwa 'RTS,S/ASO' yaliwasilishwa kwa Shirika la Afya Duniani (WHO), inayoendelea kufanyiwa kazi kwa karibu, kabla ya kupatiwa leseni kuruhusu matumizi yake kwa watu umma unaosumbuliwa na maradhi hayo duniani.

"Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha ongezeko kubwa la maambukizi ya malaria kwa watoto wenye umri wa kwenda shule, kuanzia miaka sita hadi 14m" anasema na kuongeza:

"Kwa kutambua hilo NIMR Tanga kwa kushirikiana na wadau wengine tunaendelea kufanya majaribio ya madawa mseto ya malaria... "

Kaimu Mkurugenzi huyo anasema utafiti unawalenga zaidi watoto wanaoenda shule, iwapo wakitumia dawa mseto zitawasaidia kupunguza maambukizi ya malaria, upungufu wa damu na kuboresha ufahamu wao shuleni.

"Tunaamini kwamba utafiti huu utakapokamilika utatoa takwimu zitakazosaidia Wizara ya Afya,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kufanya maboresho ya sera zinazolenga kukinga kundi kubwa la watoto," anasisitiza.

**KUNDI LA PILI**

Dk.Chiduo anasema kundi la pili la waathirika wa malaria ni kinamama wajawazito, ambao baadhi yao hujifungua watoto wenye uzito mdogo, upungufu wa damu, watoto kufika tumboni na hata mama kupoteza maisha.

Anasema matumizi ya dawa kinga wakati wa ujauzito yanaweza kuzuia maambukizi ya malaria kwa kinamama na WHO inatoa mwongozo wa kutumia dawa maarufu ya SP (Sulfadoxine Pyrimethamine).

Dk. Chiduo anasema, Licha ya ukomo wa matumizi ya dawa hiyo kwenye matumizi ya tiba ya malaria isiyo kali, ni takriban muongo mmoja na nusu, jambo linatokana na kutokuwapo kwa tiba mbadala.

**MTAFITI NIMR**

Mtafiti wa magonjwa ya binadamu kutoka kituo cha NIMR Korogwe, Dk. Samwel Geisase, anasema baada ya kujua tatizo la mafanikio hafifu ya dawa SP dhidi ya malaria wakati wa ujauzito.

Kimsingi, anasema wanatafiti upatikanaji wa mbadala na kuna tafiti za awali zimeonyesha uwezo wa kuwakinga wajawazito na malaria, magonjwa ya mfumo wa uzazi kwa baadhi ya maeneo barani Afrika.

Dk. Geisase anasema utafiti huo unafanyika katika wilaya za Korogwe na Handeni na yatatumwa kwa WHO ili kupata miongozo ya utoaji tiba kinga dhidi ya malaria kwa wajawazito.

"Tumeshiriki tafiti mbalimbali na kubaini sababu za homa kwenye wodi ya watoto ya Hospitali ya Rufani ya mkoa ya Bombo (Tanga ), Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Korogwe Magunga na kwenye baadhi ya vijiji vya wilaya za Korogwe na Handeni," anasema mtafiti huyo.

Anasema wamewahimiza wajawazito kutumia huduma za kliniki kwa kushirikiana na waume zao, ili kuleta Mafanikio makubwa.

**MKURUGENZI JIJI TANGA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga Daudi Mayeji anasema kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba mwaka huu, kuna jumla ya kaya 96,293 sawa na asilimia 123 ziliandikishwa na kupewa kuponi kwa ajili ya kugawiwa vyandarua.

Mayeji anasema, ugawaji wa vyandarua katika mitaa mbalimbali ya jiji hilo lilianza Desemba 15 mwaka jana na takriban vyandarua 272,502 vilitarajiwa kugaiwa kwa wananchi, uandikishaji uligharimu Sh. bilioni 87.4 na Sh. milioni 43.9 kitagharamia ugawaji vyandarua.

**UFUATILIAJI**

Kituo cha NIMR Tanga, kupitia mpango wa kufuatilia wagonjwa wenye homa vijijini, kilianzisha mpango wa kuwafundisha wahudumu wa afya kwenye jamii katika kuhudumia wagonjwa wenye homa.

Ni utaratibu huo unaojulikana kwa jina Community Owned Resource Persons(CORPs), unaonyesha mafanikio makubwa, hasa katika maeneo yasiyokuwa na zahanati au yaliyoko mbali na vituo vya afya.

NIMR pia imebobea kutafiti malaria, UKIMWI, kifafa, Usubi, matende na mabusha, homa ya dengue, kipindupindu, kisukari na shinikizo la damu.

NIMR Tanga kina maabara za kisasa zinazofanya vipimo kutoa majibu ya magonjwa mbalimbali yanayotafitiwa, huku ikitambua wingi wa virusi mwilini, utambuzi wa bakteria kwenye damu na dawa zinazoweza kuwaondoa, pamoja na upimaji wa kemikali kwenye figo na ini.




Ofisi ya Korogwe inayotumika katika utafiti, ikiwa sehemu ya kituo cha NIMR mkoani Tanga. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



# Msaada wa EU kuboresha mazingira

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk.Aloyce Nzuki, amesema fedha zilizotolewa na Umoja wa Ulaya (EU), zitasaidia kuondokana na uharibifu wa mazingira.

Juzi, serikali ya Tanzania ilitiliana saini mikataba sita na umoja huo yenye thamani ya Sh. bilioni 307.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo wa matumizi endelevu ya nishati ya kupikia ambao umepata Sh . bilioni 82.2.

Dk. Nzuki alisema juzi kuwa wizara hiyo kupitia ufadhili huo, itapunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi zilizokuwa zikitumika katika nishati ya kupikia ikiwamo kuni na mkaa.

Alibanisha kuwa wizara umepata ufadhili wa kutekeleza programu mbili ambazo ni mradi wa nishati na mnyonyoro wa thamani wa ufugaji nyuki.

"Programu ya kuwezesha upatikanaji wa njia mbadala ya nishati ya kupikia, lengo la miradi yote ni kuimarisha mchango wa sekta ya ufugaji nyuki kwenye ukuzaji uchumi wa nchi pamoja na kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi yanayochangiwa na ukataji miti kwa ajili ya nishati ya kupikia,"alisema.

Katibu Mkuu alibainisha kuwa programu hiyo itatekelezwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Shinyanga, Singida kwa Tanzania Bara na Kisiwa cha Pemba kwa upande wa Zanzibar.

"Katika utekelezaji wa programu hii, kazi zitakazofanyika ni kufanya mapitio ya sera, sheria na miongozo mbalimbali ya sekta ya ufugaji nyuki, kuimarisha miundombinu ya vituo vya utafiti wa ufugaji nyuki na taasisi nyingine za kisekta," alisema.

Pia alisema uanzishaji na usimamizi wa hifadhi za nyuki, kuhamasisha na kutoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki.

"Kuwezesha uanzishaji na uboreshaji wa vituo vya kukusanyia na kuchakata mazao ya nyuki na kujenga uwezo wa taasisi zinazosimamia viwango vya ubora wa mazao ya nyuki," alisema. Kuhusu nishati mbadala ya kupikia, alisema mradi huo utatekelezwa kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Tabora na Tanga.

"Kwenye huu mradi utaimarisha mifumo ya kisheria inayohusu usimamizi wa rasilimali za misitu na kujengea uwezo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania(TFS)," alisema.

Alizitaja kazi zingine kuwa ni kuimarisha huduma za ugani za misitu, kuandaa miongozo ya kiufundi ya usimamizi endelevu wa misitu, kuwezesha uanzishaji na urasimishaji wa mafunzo kwa wazalishaji wa mkaa na kuwezesha ushiriki wa wanawake wajasiriamali katika mnyororo wa thamani ya bidhaa za misitu.

Aliongeza kazi zingine kuwa ni kurejesha uoto ulioharibiwa katika misitu na kuanzisha Mfuko maalumu kwa ajili ya kuwezesha uingizaji sokoni nishati mbadala na kuhimiza matumizi yake na kuwezesha jamii kuanzisha viunga vya miti.



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndungulile (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma juzi, kuhusu ujenzi wa jengo la makao makuu ya Posta Afrika, litakalojengwa jijini Arusha. Kushoto ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Zainabu Chaula na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mashirika ya Posta Afrika, Younouss Djibrine. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Malawi yaipongeza Tanzania uratibu NGO

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

SERIKALI ya Malawi imepongeza Tanzania kwa uratibu wa mashirika yasiyo ya Kiserikali(NGOs) ili kuchangia katika maendeleo ya taifa.

Pongezi hizo zilitolewa jijini hapa na Waziri wa Jinsia, Maendeleo na Ustawi wa Jamii wa Malawi, Patricia Kaliati, wakati wa ziara ya mafunzo kuhusu hatua zinazochukuliwa na vyombo vya uratibu na uend eshaji wa NGO na kufanikiwa katika mpango wa kuwawezesha wananchi wake.

Waziri Kaliati alisema Tanzania imepiga hatua kubwa ya maendeleo katika shughuli mbalimbali pamoja na uratibu wa kazi za mashirika hayo.

"Nasi tumekuja kujifunza njia gani mnazitumia kuratibu mashirika hayo na hatimaye kuchangia katika maendeleo ya Watanzania," alisema Kaliati.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. John Jingu, alibainisha kuwa serikali imekuwa ikifanya mazungumzo ya mara kwa mara na wadau ikiwamo mashirika hayo ili kuhakikisha shughuli zinazofanyika zinakuwa na mchango mkubwa kwa Jamii.

Pia alisema Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imefanyiwa mabadiliko kadhaa ili kuhakikisha serikali na NGO zinajenga uelewa wa pamoja kuhakikisha shughuli za serikali zinawafikia wananchi kwa malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

"Ili kufanikisha mipango inayohusika kati ya serikali na NGO kuna mabadiliko mbalimbali katika sheria ya mashirika ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na uelewa wa pamoja na kuondoa malalamiko yanayoweza kujitokeza," alisema.

Alitaja siri ya mafanikio yaliyofikiwa ni kufanya ufuatiliaji kuhakikisha kwamba NGO zinafanya kazi kwa mujibu wa usajili wake.

Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Dk. Richard Sambaiga, alisema jukumu na uratibu linahitaji umakini mkubwa ili kulinda maslahi ya taifa badala ya maslahi binafsi.

"Lazima kuhakikisha kwamba kila upande unafanya kazi kulingana na malengo yake ambayo yamewekwa vinginevyo mara chache utasikia malalamiko kwamba mashirika yanaminywa," alisema.

Awali, akiwasilisha mada kuhusu sera na mfumo na uratibu wa NGO Tanzania Bara, Msajili wa Mashirika hayo, Vickness Mayao, alisema utaratibu uliopo ni kuhakikisha kwamba kuna uwazi na uwajibikaji katika uendeshaji na uratibu wa mashirika hayo.

Alisema matumizi ya mfumo wa kidigitali wa mawasiliano umerahisisha utendaji na kupunguza gharama za uendeshaji kutokana na shughuli zote kufanyika kwa njia ya mtandao.

# Kiongozi Anglikana akemea utegemezi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Kanisa Aglikana Tanzania (ACT), Mchungaji Dk. Mecka Ogunde, amewataka Watanzania kujijengea dhana ya kujitegemea na kuacha utegemezi wa misaada kutoka mataifa mengine.

Dk. Ogunde aliyasema hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akifunga mafunzo ya Vikoba kwa kimama wa kanisa hilo kutoka mikoa mbalimbali nchini.

"Ni wakati sasa sisi Watanzania kuanza kujitegemea na kuacha kutegemea misaada kutoka kwa mabeberu, maendeleo ya taifa letu yataletwa na sisi wenyewe bila kutegemea mtu mwingine au taifa lingine," alisema Dk.Ogunde.

Aidha alisema kanisa limeamua kubuni mafunzo hayo kwa ajili ya vikoba, ili kuwajengea uwezo waumini wake kujitegemea na kuinua uchumi wa familia zao na kanisa kwa ujumla.

"Dhana ya kujitegemea kama taifa tulianza nayo muda mrefu sana toka wakati wa hayati baba yetu wa Taifa mwalimu Nyerere wakati ule tulipoanzisha adhimio la Arusha hivyo tunapaswa kama taifa kujitegemea na si kutegemea mabeberu,"alisema Dk. Ogunde

Katibu mkuu huyo alisema ni aibu kwa miaka yote tangu kupata uhuru Watanzania kuendelea kuwa tegemezi kwa mataifa mengine wakati ziko rasilimali za kutosha katika taifa.

Alisema ni lazima watu wabadilike kwa kutambua fursa zilizopo na kutumia rasilimali ambazo mungu amelipatia taifa kama vile, ardhi ya kutosha, madini misitu na zingine.

"Pia kama kanisa tunasisitiza kuwa rasilimali ambazo Mungu amelijalia taifa letu zitumike kumunufaisha kila mmoja wetu na siyo kikundi fulani cha watu,"alisisitiza Dk. Ogunde.

Katibu wa Ushirika wa Kinamama Wakrito Kanisa la Anglikana (UMAKI), Magreth Masawa, alisema kupitia mpango wa 'MU Vikoba' ulio chini ya kanisa hilo, tayari wameunda vikundi 234 vyenye wanachama 5,023.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo akina mama kujiwekea akiba, kutambua namna ya kutumia fursa zilizipo katika jamii zao na kubuni miradi mbalimbali ya kuwaongezea kipato.







Baadhi ya mafundi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-UWASA), wakichimba mtaro wa kusafirisha maji machafu kwenye chanzo cha maji cha Nzovwe jana, ili kukiboresha na kufikisha maji kwenye Kata za Isyesye na Itezi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Machinga waamriwa kuhamia eneo rasmi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imeagiza wafanyabiashara wadogo maarufu kwa jina la machinga kuondoka katika maeneo yote ambayo sio rasmi kwa biashara kuanza kuondoka kwenda katika eneo la Uwanja wa Ndege wa zamani ambako kumetengwa kwa ajili yao.

Akizungumza jana kwenye kikao kati ya wamachinga hao na watendaji wa Jiji la Mbeya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema wajasiriamali hao wataondoka kwenye maeneo wanayofanyia shughuli hizo kwa lazima endapo watakaidi.

Alisema mpaka kufikia Machi 30, mwaka huu, hakuna machinga atakayetakiwa kuonekana kwenye maeneo ambayo sio rasmi ikiwamo kwenye maeneo ya hifadhi za barabara.

Chalamila alisema wanaofanya biashara zao kwenye kituo cha mabasi cha Nanenane watatakiwa kubaki huko, lakini kwa wale ambao wapo kwenye maeneo mengine yote watatakiwa kwenda Uwanja wa Ndege wa zamani.

"Mtaenda huko kwa 'modality' (njia) mbili, ya kwanza ni kusikiliza hili tangazo langu nay a pili ni kwa wale ambao watakaidi hili tangazo ambao wataenda huko kwa lazima, nayasema haya kwa sababu najua wapo wakorofi," alisema Chalamila.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwenda kuchukua Sh. milioni 100 ofisini kwake kwa ajili ya kufanyia maboresho ya eneo hilo ambalo wamachinga wanatakiwa kuhamia ili kuondoa malalamiko.

Alimtaka kumpelekea mchanganuo wa namna fedha hizo zitakavyotumika kuboresha eneo hilo ikiwamo ujenzi wa vyoo, kupeleka vifusi na mambo mengine ili kuondoa vikwazo vyote vilivyopo katika eneo hilo.

Aidha, alisema hakutaka kuwashirikisha viongozi wa machinga kwa sababu sikutaka kusumbua mtu wa aina yoyote na naagiza kule utengenezwe uongozi wa soko ambao utakuwa kiunganishi kati ya sekikali na wafanyabiashara.

Chalamila alisema baada ya Machi 30 hakuna mjasiriamali atakayekuwa anaruhusiwa kupanga bidhaa zake chini ama kuzitundika barabarani na badala yake wote watatakiwa kuelekea kwenye eneo hilo.

Alisema ili kuhakikisha biashara katika eneo hilo zinakuwa na mzunguko mzuri, magari yote yanayofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Mji wa Tunduma zitatakiwa kuhamia katika eneo hilo kutoka stendi kuu.

Baadhi ya wajasiriamali waliohudhuria mkutano huo, walishukuru serikali kwa kuweka utaratibu huo wakidai kuwa utawasaidia kufanya kazi kwa uhuru badala ya kuhatarisha maisha yao kwenye hifadhi ya barabara.

Mmoja wa machinga hao, John Simwenga, alisema awali walikuwa wanashindwa kwenda katika eneo hilo kwa sababu ya mzunguko mdogo wa biashara pamoja na ubovu wa miundombinu mibovu ya barabara.

Alisema sasa wana uhakika kuwa watafanya biashara kwa sababu mazingira yatakuwa yameboreshwa na hata wateja haitakuwa tatizo kwa sababu mabasi ya kwenda Tunduma na Chunya yataanzia eneo hilo.

"Barabara ilikuwa mbovu sana na hata baadhi ya maeneo maji yalikuwa yanajaa sana, sasa hivi tunaamini patakuwa pazuri kwa sababu serikali imeamua kuingilia kati kupaboresha," alisema Simwenga. Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, aliahidi kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa ili kulifanya Jiji hilo kuwa na utaratibu mzuri wa shughuli za wamachinga.

Kadhalika, Chalamila aliagiza Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) kuweka utaratibu mzuri wa magari kuingia kwenye eneo hilo.

# Waganga wakuu mkoa, wilaya wapewa 'meno'

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZIKIWA zimepita siku kadhaa tangu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, amsimamishe kazi Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, kwa madai ya kukiuka miiko ya kazi ya kutoa habari bila mamlaka, wizara imetoa maelekezo mapya. Mganga huyo alitoa taarifa hizo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani juu ya uwapo wa ugonjwa usiojulikana katika Kata ya Ifumbo.

Maelekezo mapya yametolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya hiyo, Prof. Mabula Mchembe, akiwa mkoani Mbeya katika ziara ya kutembelea Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya na kuzungumza na wataalamu pamoja waganga wakuu wa wilaya zote za Mkoa wa Mbeya. Prof. Mchembe aliwaagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanatoa taarifa zote za afya katika maeneo yao kwa viongozi wa kisiasa na kwenye jamii.

Alisema ni wajibu kwa kila mganga mkuu kutoa taarifa zinazohitajika kwenye jamii ili wafahamu mambo yanavyokwenda kwa sababu ni haki ya kila mwananchi kupata taarifa.

"Ni utaratibu kwamba kila mganga mkuu wa Wilaya na Mkoa kutoa taarifa zinazohusu masuala ya afya kwenye eneo lake ili kuwasaidia wananchi kupata taarifa kuhusu masuala fulani ya afya... aidha, taarifa hizo zinaweza kutolewa pia kwa wanasiasa au viongozi wengine, hivyo tumieni mamlaka hiyo kuhabarisha umma," alisema Prof. Mchembe.

Pia Prof. Mchembe aliwatoa hofu Watanzania kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 akisema ugonjwa huo sio mpya, bali ni aina ya mlipuko kama ilivyo mingine na hutokea duniani, hivyo wasikubali kutishiwa na watu badala yake waendelee kuchukua tahadhari kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema wananchi waendelee kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya na kuondoa woga kwani Covid-19 ni ugonjwa kama ulivyo mwingine na unatibika.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema hospitali hiyo inaendelea kuwahudumia wagonjwa wa aina mbalimbali ambapo hadi sasa jumla ya wagonjwa 24 wenye changamoto ya kupumua wanaendelea kupata matibabu.

Alisema hospitali hiyo ina vifaa mbalimbali vya kuhudumia wagonjwa pamoja na wataalamu waliobobea jitihada ambazo zinafanywa na serikali katika kuwahudumia wananchi wake.

Akizungumzia uvumi kwa kwenye mitandao ya kijamii kwamba Hospitali za Mkoa wa Mbeya hazina mashine za oksijeni, Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, alisema jumla ya mashine 39 zimegawanywa kwenye hospitali mbalimbali za mkoa huo na zinaendelea kufanya kazi.

Alisema taarifa zinazozagaa kwenye mitandao ya kijamii zina lengo la kuuchafua mkoa na kuwatia hofu wananchi.

Alishauri yeyote mwenye dalili za ugonjwa afike kwenye vituo vya kutolea huduma ili kupata matibabu.

# Wafugaji Mbarali waelewa suluhu migogoro ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAFUGAJI wa Wilaya ya Mbarali, wameshauriwa kununua ardhi kwa ajili ya kuchungia mifugo yao badala ya kutegemea maeneo yaliyotengwa na serikali ili kuondokana na migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, alisema wakati akizungumza na Nipashe na kutumia nafasi hiyo, kuwataka wafugaji kuacha tabia ya kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ili kuepusha migogoro, ambayo husababisha mapigano ya mara kwa mara.

Alisema maeneo yaliyotengwa na serikali hayatoshi kwa ajili ya matumizi ya wafugaji na wakulima, hivyo kufanya maeneo yaliyotengwa na Serikali na makazi ya watu kuvamiwa.

"Mfugaji ambaye umeamua kufuga mifugo mingi unatakiwa ununue ardhi yako na hiyo itasaidia kuhifadhi na kutunza mazingira kwa sababu kila mmoja atakuwa na uchungu, sitakubali kuona maeneo yaliyotengwa na serikali yanaharibiwa kwa ajili ya shughuli za kilimo na mifugo," alisema Mfune.

Baadhi ya wafugaji walimweleza Mfune matatizo yanayowakabili ikiwamo uhaba wa maeneo ya kuchungia huku wakiomba serikali kulifuta Tangazo lake namba 28 la mwaka 2008 (GN 28) ambalo lilipanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, hivyo kupunguza maeneo ya kuchungia.

Mmoja wa wafugaji hao, Shaban Olelenganunu, ambaye ni mfugaji wa Kijiji cha Mwanavala, alisema Kijiji hicho kina eneo la wafugaji ambalo lilipimwa wakati wa uwekaji wa matumizi bora ya ardhi, lakini limevamiwa na wakulima.

Alisema hali hiyo imewafanya wafugaji kukosa maeneo ya kuchungia na kwamba wakitaka kuchungia katika eneo hilo inaibuka migogoro na wakulima ambao alidai ndio wavamizi.

"Sisi wafugaji tunakuwa kama hatuhitajiki katika Wilaya hii, watu wa Tanapa wanatuzuia kuchungia kwenye hifadhi, wakulima nao wamevamia eneo letu lakini hakuna hatua zilizochukuliwa na Serikali," alisema Olelenganunu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbarali, Hashim Mwaliaga, alimuomba Mkuu wa Mkoa kusaidia kufikisha kilio cha wananchi wa wilaya hiyo ili mipaka ya hifadhi irekebishwe.

Alisema GN 28 ndio chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi katika wilaya hiyo kwa maelezo kuwa imechukua maeneo mengi ya wananchi wilayani humo na kuyafanya kuwa sehemu ya hifadhi.



# HABARI ZANZIBAR

## JUWAWAZA yakosoa uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wanawake wenye ulemavu Zanzibar (JUWAWAZA) imesema elimu ya mpigakura iliyotolewa katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana haikuwafikia walengwa wengi hasa watu wenyeulemavu.

Hayo yalielezwa jana mjini Zanzibar na Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Salma Saadat, alipokuwa akiwasilisha ripoti ya uangalizi ya uchaguzi mkuu kwa waandishi wa habari, baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Alisema watu wenye ulemavu hawakuweza kushiriki katika mikutano ya kampeni kwa sababu ya mazingira kutokuwa rafiki kwao.

Alisema kwa mfano, watu wenye ualbino hawakuwa na vivuli maalum kwenye uwanja wa kampeni ili kuwalinda na jua kali, lakini pia katika mikutano hiyo hakukuwa na watalamu wa lugha ya alama. "Pia maeneo ya maegesho ya magari yaliotengwa yalikua mbali hivyo ilikuwa shida kwa watu wenye ulemavu wa viungo kufika katika viwanja vya mikutano ya kampeni," alisema.

Alisema katika baadhi ya vituo vya kupigia kura watu wenye ulemavu walisumbuliwa na askari waliokuwa katika vituo hivyo, wakidai kutovitambua vitambulisho vilivyotolewa na ZEC kwa watu wenye ulemavu.

Jumuiya hiyo ambayo ilikua ni miongoni mwa waangalizi wa uchaguzi, ilipendekeza mambo mbalimbali ili kuhakikisha kuna uchaguzi ulio wazi na unaoaminika.

Akitaja baadhi ya mapendekezo hayo, alisema ZEC inapaswa kufanya kazi kwa karibu na asasi za kiraia zilizoidhinishwa na wadau wengine wa uchaguzi katika utoaji wa elimu ya uraia ili uchaguzi kufanywa kwa kuzingatiwa haki za binadamu.

Alisema ZEC inapaswa kufanya kazi na vyama vya siasa ili kuona ni jinsi gani wanaweza kushinikiza ujumuishaji wa wanawake na walemavu kuingia katika uchaguzi kama wagombea.

Kadhalika, alisema vyama vya siasa viimarishe utendaji wa kidemokrasia kupitia mazungumzo na kutatua kero za uchaguzi kwa njia ya amani na ya makubaliano.




Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Muhammed Mussa, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi huko Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mchakato uchunguzi ununuzi wa meli waanza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), ipo katika uchunguzi wa mchakato wa ununuzi ya meli ya MV Mapinduzi namba mbili ambayo kwa sasa haifanyi kazi za kutoa huduma kati ya Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akijibu suali la Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe, Pemba Habib Ali Moihamed, aliyetaka kujua kazi zinazofanywa na ZAECA kwa sasa katika kupambana na matukio ya ubadhirifu wa mali za umma.

Waziri Suleiman alisema Mamlaka imeanza kuwahoji watendaji wa Shirika la Meli, wakiwamo waliohusika na mchakato mzima wa manunuzi wa meli hiyo.

Alikiri kwamba meli hiyo haifanyi kazi kama ilivyokusudiwa kutoa huduma za usafiri wa uhakika kwa wananchi wa Unguja na Pemba ikiwamo kusafirisha mizigo.

Alisema meli haifanyi kazi kwa muda wa miaka mitatu tangu iliponunuliwa mwishoni mwa mwaka 2015, jambo ambalo limeibua malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na kuhoji sababu zilizosababisha meli hiyo kushindwa kufanya kazi.

"Mheshimiwa Spika, kazi za Mamlaka ni kufichuwa matukio yote ya rushwa kutoka kwa watendaji wa Serikali wasiokuwa waaminifu...napenda kulijulisha Baraza la Wawakilishi kwamba watendaji wa ZAECA wameanza kuwahoji watendaji waliohusika kufanya manunuzi ya meli hiyo," alisema.

Alieleza kuwa watendaji wa ZAECA wanapitia nyaraka zote za manunuzi ya meli hiyo.

Aidha alisema watendaji watakaobainika kufanya hujuma na kuisababishia hasara Serikali katika kufanya manunuzi ya meli hiyo, watachukuliwa hatua za kisheria.

"ZAECA haitamuonea mtumishi wa Serikali ambaye hahusiki na kufanya vitendo vya ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha za Serikali...waliohusika ndiyo watakaochukuliwa hatua za kisheria," alisema Waziri huyo.

## Wakala wa JKU watoa huduma ulinzi vituo 104

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ, Masoud Ali Mohamed, amesema wakala wa ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU), imefanikiwa kutoa huduma za ulinzi katika vituo 104, zikiwamo hoteli za kitalii na ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti maalumu, Mwanaidi Kassim Mussa, aliyetaka kujua kazi za wakala wa ulinzi wa JKU.

Masoud alisema wakala wa ulinzi wa Jeshi la kujenga uchumi (JKU) umeundwa kwa mujibu wa sheria nambari 6 ya mwaka 2019 ambayo kulinda mali za wawekezaji na watalii.

Alisema wakala huo umeanza vizuri kwa kupata kazi za ulinzi wa maeneo 104 ikiwamo hoteli za kitalii na Ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema mahitaji ya kulinda maeneo ya hoteli pamoja na miradi ya wawekezaji ni makubwa ambapo yapo maeneo 250 yanahitaji huduma za ulinzi.

Hata hivyo, alisema wakala wa ulinzi wa JKU kwa sasa hana uwezo wa kutoa huduma za ulinzi kwa sababu mbali mbali ikiwamo uhaba wa vyombo vya ulinzi na doria.

"Wakala wa ulinzi wa JKU ni taasisi ambayo tumeipitisha kwa mujibu wa sheria ya Baraza la Wawakilishi kutoa huduma za ulinzi kwa taasisi za Serikali na sekta binafsi ikiwamo wawekezaji na hoteli za kitalii...tunatoa huduma katika maeneo 104 lakini mahitaji yapo zaidi ya maeneo 250," alisema.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kuchukua mikakati ya kuimarisha wakala wa ulinzi wa JKU kwa kutoa vifaa vya kazi za ulinzi kwa ajili ya kuleta ufanisi zaidi.

Mohamed aliwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba fedha zinazotokana na mapato ya ulinzi kutoka kwa taasisi na sekta mbali mbali za Serikali na binafsi zinapelekwa hazina.

"Sina takwimu halisi ya mapato yaliyokusanywa yanayotokana na huduma za wakala wa ulinzi kutoka kwa taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano pamoja na sekta binafsi...nitaleta hapa kwa maandishi," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA SHULE**

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano :0713327613.

Uza,
Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Simon Peter Jonathan** ambaye ni msimamizi wa mirathi ya Marehemu **Peter Edwin**. Anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja namba **241, Kitalu "LL" (HD)** Lubaga Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi Kilichopo Karibu au awasiliane na Simon Peter Jonathan kwa simu namba **0658842928. RB NAMBA/SHY/RB/2021.** Control Namba **9910820226873.**

Muho Motungu
AFISA ARDHI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLUTHER ABDALLAH NUNGU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 659 DKX** aina ya **TOYOTA NOAH** chasis namba **SR500095820** engine namba **358064060**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa DAR/MAG/RB/92254/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**HUMPHREY MWETENI** anatangaza kupotelewa kwa vyeti vifuatavyo,cheti cha kidato cha nne chenye index namba **CS No.0410998** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **AZANIA** mwaka **2004** na cheti cha kidato cha sita index namba **ACS No.0214294** kilichotolewa mwaka 2007 na shule ya secondary **AGAPE LUTHERAN J SEMINARY** ,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/MBA/RB/84292/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA
DODOMA
Shuri la Rufaa Jinai/Madai/Talaka /Mirathi/Maombi na. 81/2020
Katika Mahakama ya WILAYA DODOMA
Jinai/Madai/Talaka /Mirathi/Maombi Namba. 81 Mwaka 2020**

**ADAM SWAI……………….Mrufani/Mwombaji
Dhidi ya
PHILIPO KAPANDE…….Mrufaniwa/Mjibu Maombi**

**KWA:PHILIPO KAPANDE**

Kwa kuwa Rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa/ itatajwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya **IJUMAA Tarehe 19/2 mwaka 2021** Mbele ya **Mhe.R.J. MAGOTI** unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo vyako vyote kama vipo
Hati hii inatolewa kwa amri yangu na Mhuri wa Mahakama hii leo
**Tarehe 15 mwezi 02,2021**

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA
DODOMA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
katika Mahakama ya Mwanzo CHAMWINO MJINI
Wilaya ya DODOMA
TALAKA MADAI NAMBARI 06/2020**

**MDAI…………………………SPELANZIA PIUS KIWESI
DHIDI YA
MDAIWA……………………GERALD CLAUD MZWA**

**KWA GERALD CLAUD MZWA**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya **JUMANNE tarehe 23/02/2021 saa 08:00** asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **09/02/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MÀHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA MADAI NO 53/2021**

**MDAI: CHRISTOPHER PAULO KUCHERA
DHIDI YA
MDAIWA: EBRANIA MAHUMBO**

Ombi la Mdai: **CHRISTOPHER PAULO KUCHERA**
Madai ya pesa Tsh 420,000/-
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauril tajwa hapo juu bila kukosa.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 4 Mwezi 3 Mwaka 2021 saa 8:30 Asubuhi/ Alasiri.

Angalia Kama hukuhudhuria/hamtohudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha Kama Umepokea/ Mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Màhakama hii leo tarehe 16 Mwezi 2 Mwaka 2021.

**HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA TARAKA NO 19/ 2021**

**MDAI JOVIN MKUCHU
MDAIWA MARY LOGGA**

**Ombi la Mdai JOVIN MKUCHU**

**Madai ya TALAKA**
Unatakiwa kuhudhuria hapa mahakamani katika SHAURI tajwa hapo juu bila kukosa. Shauril limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 2 mwezi 3 mwaka 2021Saa 2:30 Asubuhi/ Alasiri.
Angalia Kama* hukuhudhuria/hamtohudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Màhakama Ikithibitisha Kama umepokea/ mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu Kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Màhakama hii leo tarehe 17 mwezi 2 mwaka 2021

**HAKIMU
MÀHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIA (MCA/63)
Mahakama ya mwanzo ARUSHA MJINI
Wilaya ya ARUSHA NAMBARI 146 YA 2020**

**Mdai… JULIANA ELIREHEMA RAPHAEL
Amdai
Mdaiwa ..ISMAIL MAJID
Kwa ISMAIL MAJID
NJIRO - ARUSHA**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) **UNATAKIWA KUHUDHURIA MAHAKAMANI HAPA BILA KUKOSA ILI KUJIBU MADAI YA FEDHA SH: 1,670,000/=**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe J.TANO tarehe 3/3/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo kwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, mahakama ikithibitisha kama umepokea /mmepokea kwitwa shaurini hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 10/2/2021

………………………………………..
Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo .

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AJUAYE ABSALOM VEGULA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajili **T 286 AUG** chasis namba **TES3ECS50391** engine namba **4364**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa DAR/CHA/RB/88141/2021**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 -0782253676

## TEGEMEZA & COURT BROKER LIMITED
## NOTISI/MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na Benki ya NMB tunatoa notisi ya siku kumi nan ne (14) kuanzia tarehe 18/02/2021 hadi tarehe 04/03/2021. Wadaiwa waliotajwa hapa chini walipe madeni yao. Endapo watashindwa kulipa kwa muda uliotajwa dhamana zao zitauzwa kwa mnada wa hadhara kwa ratiba ifuatayo:

| JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA | ENEO NA NAMBA YA KIWANJA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| BIAGATI SEA FOOD CO. LTD & MDHAMINI VENANCE LUTABISHA MONZI | KIWANDA CHA SAMAKI NA MASHINE ZAKE | TABATA ST. MARY PLOT No. 540 BLOCK 'A' | 06/03/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| BAB G ONE CO. LTD MDHAMINI JOHN PETER MWACHA | NYUMBA GHOROFA 1 | KIGAMBONI KISARAWE II PLOT NO. 120& 122 | 07/03/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**
1. UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI
2. MALIPO NI 25% YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA SALIO LITALIPWA NDANI YA SIKU 14.
3. ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOTOLEWA, ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE NA NYUMBA ITAUZWA TENA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NA. 0719 187677 / 0762 443118**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Viongozi wa uasi CAR wafikishwa ICC

**Bangui, CAR**

VIONGOZI wawili wa kundi la uasi la kikristo katika Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), wamekana mashtaka ya uhalifu wa kivita pamoja na ukatili wa kibinadamu katika kesi yao, mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC).

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la AP, aliyekuwa ofisa wa soka Patrice Edouard Ngaissona na Alfred Yakatom ambaye ni kiongozi wa uasi anayejulikana kama Rambo, wanatuhumiwa kuhusika kwenye mauaji, mateso pamoja na mashambulizi dhidi ya raia.

Mashtaka hayo ni kutokana na nafasi zao za uongozi kwenye kundi la uasi la kikristo la anti-Balaka lililoshutumiwa kuhusika kwenye mapigano makali na kundi la kiislamu la Seleka kati ya mwaka 2013 na 2014.

Mapambano hayo yalisababisha vifo vya maelfu ya watu huku wengine wakikoseshwa makazi, misikiti pamoja na maduka yakiporwa.

Mashtaka yaliyosomwa juzi, ni ya kwanza mbele ya ICC yanayoangazia ghasia zilizotokea baada ya kundi la Seleka kutwaa madaraka mwaka 2013, yaliyosababisha Rais wa wakati huo, Francois Bozize, kutorokea uhamishoni.

***VOA***




Waandamanaji waliokusanyika karibu na eneo la Sule Pagoda kupinga mapinduzi ya kijeshi, Myanmar, jana. UN ilionya kuwa wanajeshi wanaoletwa Yangon na kwingineko wanaweza kuashiria uwezekano wa vurugu kubwa. **PICHA:AP**

# Libya yamkumbuka Muammar Gadhafi

**Tripoli, LIBYA**

RAIA wa Libya, wanaadhimisha miaka 10 tangu yalipoanza maandamano ya wananchi na kusababisha kuuawa na kuondolewa madarakani kwa kiongozi wa nchi hiyo, Muammar Gadhafi.

Maadhimisho hayo yanafanyika wakati wananchi wa Libya, wakiweka matumaini yao kwa serikali mpya, iliyo na kazi ya kuongoza nchi hiyo kuwa na uchaguzi baadaye mwaka huu.

Miaka kadhaa sasa, Umoja wa Mataifa (UN), umekuwa ukiongoza mazungumzo kati ya pande zote pinzani kusaidia kuleta amani na utulivu nchini humo.

Wapiganaji wa kigeni pia wanatakiwa kuondoka na silaha huku zikizuiwa kuingizwa nchini humo, masuala ambayo bado hajatekelezwa.

Hata hivyo, maadhimisho hayo yanafanyika wakati nchi hiyo ikiendelea kuwa na serikali mbili, moja inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa jijini Tripoli na inayoongozwa na makundi ya wapiganaji chini ya Jenerali Khalihaf Haftar.

Ripoti ya Shirika la Kimataifa ya Amnesty International katika ripoti yake, imeendelea kushinikiza kuchukuliwa hatua kwa wale wote waliohusika na visa vya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa kipindi chote cha miaka 10.

***RFI***

## Korti Rwanda kusikiliza kesi ya Rusesabagina

**Kigali, RWANDA**

MAHAKAMA ya Rwanda hii jana, ilianza kusikiliza kesi dhidi ya Paul Rusesabagina na wengine 20 wanakabiliwa na mashtaka ya ugaidi.

Rusesabagina, mkosoaji wa Rais Paul Kagame, anatuhumiwa kuunga mkono shughuli za kikosi cha National Liberation (FLN), ambacho ni mrengo wa wanamgambo wa chama chake cha Rwandan Movement for Democratic Change (MRCD).

Alikamatwa Agosti mwaka jana, akiwa katika nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kurudishwa nchini Rwanda kukabiliana na mashtaka ya ugaidi, utekaji nyara na mauaji.

Julai mwaka 2018, FLN ilidai kuhusika na mashambulio katika mkoa wa kusini wa Rwanda.

Rusesabagina alifahamika kufuatia filamu ya Hotel Rwanda ikielezea jinsi alivyookoa maisha ya Watutsi waliokuwa wamekimbilia katika hoteli moja mjini Kigali aliyokuwa meneja wake mwaka 1994.

Rais Paul Kagame alisema kikubwa sio ushujaa wa Rusesabagina au vitendo vyake wakati wa mauaji ya kimbari, kinachoangaliwa sasa ni yeye.

"Kuna maswali ambayo lazima atayajibu, kuna wanaomsaidia wakiwa Ulaya, Marekani na kwingineko na ambao walimpandisha cheo na kumpa majina ya ushujaa, awe shujaa au la, mimi sina wasiwasi na hilo."

***BBC***

## Pakistan yakosoa ziara za Kashmir nchini India

**Islamabad, PAKISTAN**

PAKISTAN imekosoa ziara za mabalozi wa kigeni na wanadiplomasia, zinazotekelezwa katika eneo la Jammu Kashmir linalodhibitiwa na India.

Katika taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Pakistan, ilidaiwa kuwa ziara hizo zililenga kugeuza mtazamo wa ulimwengu kutoka kwa ukiukaji wa haki za kibinadamu uliofanywa na utawala wa India katika eneo lenye mgogoro.

Katika taarifa hiyo, ilisisitizwa kuwa wawakilishi wa kidiplomasia wataruhusiwa na kuwekewa mipaka ya ziara kwa mikoa yote kwa sharti za kuzingatia ushirikiano huru na watu wa Kashmir.

Ikibaini kuwa ziara inakusudia kuleta maoni potofu ya hali ya kawaida katika Bonde la Himalaya, wizara ilisema.

"Watu wa Kashmir wanauawa bila kinyume cha sheria katika shughuli za operesheni za utafutaji. Mateso kizuizini, ongezeko la upotevu, kuzuiliwa kwa viongozi wa Kashmir gerezani, unyanyasaji wa waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu na mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu, pamoja na ukosefu wa haki za kimsingi yote hayatambuliwi." India awali ilikuwa imeandaa ziara mbili kama hizi kwenda eneo hilo na wanadiplomasia wa kigeni.

Pakistan inaitaka India kuwaruhusu maofisa wa Shirika Kuu la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa (UN), Tume Huru ya Kudumu ya Haki za Kibinadamu na wachunguzi wengine wa UN, pamoja na vyombo vya habari vya kimataifa kumtembelea Jammu Kashmir na kutathmini hali ilivyo.

***TRT***



# ALABA
## ATANGAZA KUONDOKA BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

DAVID Alaba amethibitisha ataondoka Bayern Munich wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mlinzi huyo wa kati, Alaba alilelewa katika akademi ya Bayern na ameichezea timu hiyo kwa kipindi cha miaka 13.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, alitangaza uamuzi wake Jumanne, ingawa hakuweka wazi wapi atakakoelekea.

Alaba kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na Real Madrid, huku miamba ya Ligi Kuu England, Liverpool, Manchester City na Chelsea nazo zikitajwa kumwania.

"Nimeamua mwenyewe kufanya kitu fulani kipya baada ya msimu huu," alisema Alaba akiwaambia waandishi wa habari.

"Nitaondoka klabuni na hayakuwa maamuzi rahisi, ilikuwa ni ngumu sana kwa sababu nimekuwa hapa kwa miaka 13 na naitambua vizuri sana klabu hii, ipo moyoni mwangu na najivunia kucheza hapa.

"Bado sijaamua klabu gani nitakwenda. Hilo litatokea kwa hapo baadaye."



## MARTIAL ASHAMBULIWA TENA KWENYE MITANDAO

**MANCHESTER, England**

ANTHONY Martial, amejikuta akiingia katika wakati mgumu kwa mara nyingine baada ya kushambuliwa mitandaoni, wakati timu yake ya Manchester United ilipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya West Bromwich Albion, Jumapili.

Mfaransa huyo alianza katika kikosi cha kwanza kabla ya kutolewa dakika ya 66, baada ya timu yake kushindwa kuonyesha makali ya kufunga ili kuwafukuzia kwa ukaribu wapinzani wao, Manchester City ambao wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Baada ya mchezo huo, kulianza kusambaa ujumbe wa chuki na ubaguzi wa rangi dhidi yake zikiwa na alama na picha mbalimbali kupitia Instagram.

Hii ni mara ya pili kwa mshambuliaji huyo kushambuliwa tangu kuanza kwa mwaka huu, mara ya kwanza ilikuwa baada ya United kufungwa 2-1 na Sheffield United.

Wachezaji wengine wa Ligi Kuu ambao wamewahi kuhusika katika kushambuliwa kwa maneno kama ilivyo kwa Martial ni Reece James na Antonio Rudiger wa Chelsea na Romaine Sawyers wa West Brom.

Kumekuwa na presha nyingi juu ya watu wanaohusika kutoa kauli za kibaguzi mitandaoni, wadau wa soka wakiwamo wachezaji wakitaka mitandao husika iwafichue na ikiwezekana iwafungie.

# KLOPP AMWAGA SIFA KWA ALISSON

**LIVERPOOL, England**

ALIISSON amekalia kuti kavu, lakini sasa "atalala vizuri" kwa mujibu wa kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp baada ya kulinda lango vizuri na 'Wekundu' hao kupata ushindi wa 2-0 dhidi ya RB Leipzig, juzi Jumanne.

Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Mohamed Salah na Sadio Mane yaliiwezesha Liverpool kupata ushindi huo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 mjini Budapest, huku wakitarajia kurudiana Machi 10, mwaka huu.

Hata hivyo, pamoja na mabao hayo, Alisson alifanya kazi ya ziada kuokoa hatari langoni mwake, hasa shuti la Christopher Nkunku la dakika ya 46.

Golikipa huyo wa Brazil alishutumiwa sana wakati Liverpool wakichezea kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa Manchester City na pia kipigo cha 3-1 walichopewa na Leicester City kwenye Ligi Kuu England.

"Kwa uhakika kabisa, amefanya kazi nzuri," alisema Klopp wakati alipoulizwa kuhusu Alisson. "Alikuwa na wakati mzuri na amecheza vizuri, kwa uhakika leo (juzi) atalala vizuri sana."

## HABARI MICHEZO




# MESSI

## AIFIKIA REKODI YA RAUL ULAYA

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi ameifikia rekodi ya kufunga kwa miaka 17 mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyowekwa na gwiji wa Real Madrid, Raul.

Messi alifunga penalti dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 na kuifikia rekodi hiyo juzi, Jumanne.

Macho yote kwenye mchezo huo yalikuwa kwa Messi ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda PSG, lakini Barcelona wakajikuta wanachezea kichapo cha mabao 4-1.

Frenkie de Jong alikwatuliwa na Layvin Kurzawa na mwamuzi, Bjorn Kuipers akawapa penalti Barca iliyofungwa na Messi.

Sasa amefikia rekodi hiyo ya Raul kwenye mashindano hayo ya Ulaya wakati alipofunga kuanzia mwaka 1995 hadi 2011.

Yeye Messi alianza kufunga kwa mara ya kwanza kwenye mashindano hayo mwaka 2005 hadi sasa.

Hilo pia lilikuwa bao lake la 20 kwa Messi kwenye mashindano yote msimu huu.

## Greenwood ajifunga tena Man UTD

**MANCHESTER, England**

MASON Greenwood amesaini mkataba mpya na Manchester United ambao utambakisha pale Old Trafford hadi Juni 2025, huku kukiwa na kipengele cha kumwongezea muda zaidi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amekuwa akipangwa katika kikosi cha kwanza chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer, alicheza mchezo wake wa kwanza mwaka 2019 na tayari amecheza mechi 82.

Anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji chipukizi wenye vipaji vya juu ndani ya Ligi Kuu England, na amepewa tuzo kwa maendeleo yake na bidii na mpango mpya wa kumfanya abaki klabuni hapo kwa miaka isiyopungua minne ijayo.

Greenwood alicheza mchezo wake wa kwanza akitokea benchi kwenye ushindi wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Paris Saint-Germain Machi 2019.

Mechi yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu ilikuwa siku ya mwisho ya msimu wa 2018-19 dhidi ya Cardiff.

Greenwood amefunga mabao 21 kwa kikosi cha kwanza, na 17 yalitokea kwenye msimu uliopita wakati alipokuwa na msimu wa kuvutia baada ya kuanza tena kufuatia mapumziko kutokana na corona.

Lakini amefunga mabao manne tu kwenye mashindano yote kwa msimu huu.





# Arsenal hawajafikia mwafaka kwa Luiz

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal imeripotiwa kuwa bado haijaanza kujadiliana juu ya mkataba mpya na mlinzi wake wa kati, David Luiz.

Raia huyo wa Brazil alipewa miezi 12 kwenye mkataba wake wa msimu uliopita wa majira ya joto baada ya kumvutia kocha, Mikel Arteta kwa mchango aliokuwa nao klabuni hapo.

Mkataba wa sasa wa nyota huyu mwenye umri wa miaka 33, unaisha Juni na anatarajiwa kuondoka Arsenal mwishoni mwa msimu, huku kukiwa na taarifa kwamba 'Washikabunduki' hao




wanafikiria kumwongezea muda.

Taarifa zinaripoti kuwa kikosi cha Arsenal kinachopanga dirisha la uhamisho wa majira ya joto tayari kinaendelea na kazi, na wachezaji kadhaa pamoja na Luiz wakiwa hawana uhakika juu ya hatima yao.

Walinzi wa kati Rob Holding, Gabriel Magalhaes na Pablo Mari wote wanatoa ushindani katika chaguzi za safu ya ulinzi na wote wana umri wa miaka 27.

Luiz amecheza mara 14 kwenye Ligi Kuu hadi sasa msimu huu na vile vile alishiriki mara tatu kwenye Ligi ya Europa, akifunga mara moja dhidi ya Rapid Vienna, Oktoba mwaka jana.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE SASA ANAWATAFUTA MESSI, RONALDO - GRIEZMANN

●●●Ni baada ya kuiua Barca kwa hat-trick, asema anachoweza kufanya kwa sasa ni kumpa tu hongera kwa...

**BARCELONA, Hispania**

KYLIAN Mbappe anaweza kuwafikia Lionel Messi na Cristiano Ronaldo baada ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' wakati Paris Saint-Germain ikiifumua Barcelona, kwa mujibu wa Antoine Griezmann.

Mbappe alifunga mabao hayo matatu wakati PSG ikiifunga Barcelona 4-1 kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora pale katika dimba la Camp Nou, juzi Jumanne.

Messi alianza kuwapa Barca bao la kuongoza alilofunga kwa mkwaju wa penalti, kabla ya mambo kuwabadilikia. Mbappe alisawazisha bao hilo baada ya kazi nzuri ya Marco Verratti, kabla ya kuongeza mengine mawili na Moise Kean kufunga moja.

Baada ya mchezo huo, Griezmann alimsifia Mbappe ambaye ni mchezaji mwenzake kwenye timu ya Taifa ya Ufaransa, kwa kusema kwamba, ana safari ndefu ya mafanikio.

"PSG wana nyota mkubwa sana wa baadaye ambaye atakuwa katika daraja la Leo na Cristiano," alisema Griezmann akiiambia MC sport.

"Ninachoweza kufanya kwa sasa ni kumpa tu hongera."

Mbappe amekuwa mchezaji wa tatu kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kufunga hat-trick dhidi ya Barcelona na wa kwanza kwa kipindi cha karibia robo karne baada ya nyota wa Newcastle United, Faustino Asprilla na straika wa Dynamo Kiev, Andriy Shevchenko wote kufanya hivyo mwaka 1997. Mbappe mwenye umri wa miaka 22, alikuwa nyota wa mchezo huo kwa kutengeneza pasi nyingi kwa wachezaji wenzake.

"Tulihitaji kuwa kwenye mchezo mzuri. Lakini hatukuweza. Ni kipigo kikubwa kwetu," alisema Griezmann.

"Tulikuwa tayari, tulitaka kucheza mchezo mkubwa, lakini wao walikuwa bora zaidi ya sisi. Sina cha kusema. Kylian alikuwa na wakati mzuri."

## KWA UFUPI

**UNITED WAMTAKA VELVERDE**

MANCHESTER United inamfuatilia kiungo wa Real Madrid na Uruguay, Federico Valverde mwenye umri wa miaka 22. ***(Sun)***

**EVERTON WARUDI KWA RABIOT**

EVERTON watajaribu tena kumsajili kiungo wa Juventus na Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 25, kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

**CALETA-CAR AFUNGUKA LIVER**

MLINZI wa kati wa Marseille na Croatia, Duje Caleta-Car mwenye umri wa miaka 24, amesema alikataa kujiunga na Liverpool, Januari. ***(Goal)***

**ALABA ANAITAKA REAL MADRID**

MLINZI wa Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, anataka Real Madrid kuwa ndio timu atakayokwenda kucheza mara atakapoondoka Bayern Munich mwishoni mwa msimu huu na ameanza kujifunza Kihispania, lakini uhamisho wake kwenda pale kwenye dimba la Bernabeu utategemea na majaliwa ya mlinzi wa kati, Sergio Ramos. ***(Mirror)***

**UPAMECANO NUSURA ATUE UTD**

MANCHESTER United walikaribia kumsajili Upamecano kwa pauni milioni 1.9 mwaka 2015, kwa mujibu wa mshauri wa mchezaji huyo. ***(Mirror)***

**PULISIC, ZIYECH MMOJA KUUZWA**

WINGA wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 22, na mshambuliaji wa Morocco, Hakim Ziyech, 27, wamekuwa na wakati mgumu chini ya kocha mpya, Thomas Tuchel na mmoja kati yake anaweza kuuzwa kipindi cha majira ya joto. ***(Star)***

**MOURINHO KUOGA FEDHA**

KLABU ya Tottenham Hotspur ikimfukuza kazi kocha, Jose Mourinho inaweza kuwagharimu kiasi cha euro milioni 40. ***(A Bola)***

**NAGELSMANN, RODGER NA SPURS**

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann na kocha wa Leicester, Brendan Rodger wametajwa kurithi mikoba ya Jose Mourinho pale Tottenham endapo atatimuliwa. ***(Mail)***

**GRAY HAKUPEWA MKATABA**

WINGA wa England, Demarai Gray mwenye umri wa miaka 24, amesema kamwe hakupewa ofa ya mkataba mpya na Leicester kabla ya uhamisho wake wa kwenda Bayer Leverkusen, Januari. ***(Sky Sports)***

**MBAPPE ATOA NENO PSG**

STRAIKA wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2022, amesema ana "furaha" kwa miamba hao wa Ligue 1, lakini raia huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, amebainisha kuwa anatakiwa kufikia uamuzi kuhusu majaliwa yake. ***(RMC Sport, via Metro)***

**MADRID YAMTAKA CARMO**

REAL Madrid imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa kati wa Braga na Ureno, David Carmo. Liverpool ilijaribu kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, Januari lakini mazungumzo yalivunjika. ***(AS)***

HABARI MICHEZO

# JULIO: SABABU NGORONGORO HEROES KIPIGO KWA GHANA

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa timu ya Tanzania chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes, Jamhuri Kihwelo 'Julio', amesema makosa ya kizembe ndiyo yaliyoigharimu timu hiyo kupoteza mechi ya kwanza ya Fainali za Mataifa ya Afrika kwa vijana chini ya umri huo kwa mabao 4-0 dhidi ya Ghana juzi, kwenye Uwanja wa Stade Municipal de Nouadhibou nchini Mauritania.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, kocha huyo alisema ukiangalia takwimu za mchezo mzima timu ya Ngorongoro Heroes iliwazidi kila kitu Waghana, lakini kilichowaponza ni makosa binafsi ya baadhi ya wachezaji wake ambao walisababisha wapinzani wao kupata mabao.

"Sitaki kumzungumzia mchezaji mmoja kuwa ana makosa, nasema kuna baadhi ya wachezaji wangu walifanya makosa nasema ya kizembe tumeadhibiwa. Hatujafungwa kwa eti tumezidiwa, ukiangalia takwimu za mechi hii zote sisi tumekuwa juu yao, kwa hiyo hili limepita tunaangalia mechi ijayo," alisema Julio.

Mashabiki wengi nchini wamekuwa wakimlaumu kipa Daniel Mgore kuwa amefungwa mabao mawili mepesi ambayo hakupaswa kuruhusu kutokana na uzoefu wake wa Ligi Kuu, akiwa anaidakia Biashara United.

Alisema kwenye kundi lao, Ghana inaonekana kuwa ndiyo timu tishio, lakini Morocco na Gambia si za kutisha sana, na kwamba timu yake inaweza kupambana na kupata matokeo mazuri.

"Kama Ghana ambayo ndiyo timu bora tumeizidi kwa kila kitu, sidhani kama tutashindwa kufanya vizuri kwenye mechi mbili zilizobaki kwa sababu hawana ubora kama wa Ghana, ingawa wana baadhi ya wachezaji wazuri," alisema.

Mbali na Tanzania na Ghana, timu zingine zilizo kwenye kundi hilo la C ni Morocco na Gambia.

Ngongoro Heroes itatupa karata yake nyingine Ijumaa kwa kucheza dhidi ya Gambia kwenye uwanja huo, ambayo nayo ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Morocco juzi, Jumanne.



Kikosi cha Ngorongoro Heroes.

# Ilamfya alia kubaniwa Simba akitupia KMC

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Charles Ilamfya anayeichezea KMC kwa mkopo akitokea Simba, amefunga bao lake la pili kwa timu hiyo kwenye mechi tatu alizoicheza tangu ajiunge nayo kwenye kipindi cha dirisha dogo Januari, akidai kuwa hakuwa akipata nafasi kwenye kikosi hicho na kuaminiwa, hivyo kutoonyesha makali yake.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya KMC na Mwadui FC, akifunga bao moja lililoisaidia timu yake kushinda mabao 2-1, Ilamfya alisema anajisikia furaha kwa sababu amecheza mechi yake ya tatu akiwa na timu ya KMC na kufunga mabao mawili mpaka sasa.

"Ni kuaminiwa tu, huku wananiamini na napata nafasi. Simba unajua ni timu kubwa na ina presha nyingi kutoka nje ya uwanja, kwa hiyo mchezaji kama mimi ni ngumu sana kupata nafasi na kuaminiwa. Ni hilo tu na wala si kwamba kule kiwango changu kilishuka," alisema.

Straika huyo alianza kucheza mechi yake ya kwanza Februari 4, mwaka huu, baada ya kurejea KMC wakati ikiishindilia Namungo mabao 3-0, Ilamfya akifunga bao moja, lakini alishindwa kuziona nyavu kwenye mechi ya pili Februari 12 dhidi ya Prisons, timu yake ikilala kwa mabao 2-1, kabla ya juzi kufunga moja kwenye mechi yake ya tatu, likiwa ni bao la pili kwenye mchezo huo.

Simba ilimsajili mchezaji huyo kutoka KMC, ambapo alitamba sana, lakini hakuonyesha kile ambacho kilimfanya asajiliwe, akikumbana na changamoto ya kupata namba mbele ya mastraika hatari kama Mnyarwanda Meddie Kagere, Mtanzania John Bocco na Mkongomani Chriss Mugalu.

## ZFF yafungua rasmi usajili dirisha dogo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR.**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limefungua rasmi usajili wa dirisha dogo kwa msimu huu wa 2020-2021, ambalo litakuwa wazi kuanzia leo Februari 18 hadi Machi Mosi, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili visiwani hapa jana, Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano wa ZFF, Ali Mohammed Ameir, alisema usajili huo utafanyika kwa njia ya mtandao na utafungwa Machi Mosi majira ya saa 6:00 usiku.

Aidha, alizisisitiza timu zote kufanya usajili kwa wakati uliopangwa ili kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza kutokana na usajili huo kwa njia ya mtandao.

"Timu zifanye usajili kwa wakati, hakutakuwa na muda wa nyongeza wa usajili kwa kuwa mtandao kama unavyojua unaendana na 'setting', hivyo timu zihakikishe zinafanya usajili ndani ya muda uliopangwa.

Hata hivyo, alisema kuwa usajili huo utafanyika huku ligi zote zikiwa zinaendelea kuchezwa tofauti na misimu iliyopita ambapo kipindi cha dirisha dogo ligi hiyo ilikuwa ikisimama.

## Simba Queens kuanza na Mapinduzi Queens

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, mzunguko wa pili inatarajiwa kurejea kesho, Ijumaa baada ya kusimama kwa muda kipindi cha usajili wa dirisha dogo lililofunguwa Januria 15, mwaka huu.

Kwa mujibu ratiba, Ijumaa kutakuwa na mechi tatu ambapo mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba Queens itakuwa nyumbani kuwakaribisha Mapinduzi Queens katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju jijini Dar es Salaam.

**Mechi nyingine itakayo pigwa kesho itakuwa kati ya Baobab Queens iki wakaribisha mahasimu wao JKT Queens timu zote maskani yakiwa Dodoma ambapo mechi hiyo ita pigwa katika Uwanja wa Jamhuri, huku pia TSC Queens iliwakaribisha ES Unyanyembe.**

Ratiba hiyo inaonyesha, Jumamosi Yanga Princess ambao wameshikilia usukani wa ligi hiyo watakuwa ugenini dhidi ya Tanzanite katika Uwanja wa Fountain Gate Arena huku Alliance Girls ikiwakaribisha Kigoma Sisters katika dimba la Nyamagana jijini Mwanza.

Mpaka ligi hiyo inakwenda mapumziko Yanga Princess ilikuwa ikiongoza kileleni ikiwa na pointi 31, ikifuatiwa na Simba Queens ambao wana alama 29.

# Michezo

Alhamisi Februari 18, 2021

Nipashe




MBAPPE SASA ANAWATAFUTA MESSI, RONALDO - GRIEZMANN HABARI UK 22

ISIWE TABU...



Beki wa kati wa Barcelona, Gerard Pique, akimvuta jezi mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe baada ya kumzidi mbio wakati akikokota mpira kuelekea langoni mwao, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora iliyopigwa Uwanja wa Camp Nou na PSG kushinda 4-1. Mbappe atupia hat-trick. **PICHA: MTANDAO**

## SIMBA, AL AHLY ZASHTUA CAF

Zaweka rekodi, Waarabu watuma salamu Msimbazi, Gomes akili kwa Biashara United kwanza leo...

**Na Mwandishi Wetu**

RAUNDI ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi imebaki mechi moja tu ya Kundi C kati ya Wydad Casablanca ya Morocco na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini kukamilika baada ya juzi usiku mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri kuibuka na ushindi kwenye mechi ya Kundi A dhidi ya wageni wao, Al-Merrikh ya Sudan.

Mechi ya Wydad Casablanca na Kaizer Chiefs haijafanyika kutokana na Serikali ya Morocco kuzuia wageni wote kutoka Afrika Kusini kuingia nchini humo kwa sababu ya kuhofia kuenea kwa virusi vipya vya corona vilivyoanzia Sauzi.

Hata hivyo, hadi sasa kundi linaloonekana kuwa gumu na kushtua makundi mengine kwenye michuano hiyo ya CAF, hadi sasa ni Kundi A, ambalo linaundwa na Al Ahly, Al-Merrikh, AS Vita ya DR Congo na Simba ya Tanzania.

Hadi sasa kundi pekee ambalo kuna timu mbili zilizoibuka na ushindi ni Kundi A, ambapo Simba ilishinda bao 1-0 dhidi ya AS Vita ugenini huku Al Ahly juzi nayo ikiwa nyumbani katika Uwanja wa Kimataifa wa Cairo ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Al-Merrikh, hivyo kuanza kutoa picha ya mbio ngumu za farasi wawili.

Kundi B Mamelodi Sundowns inaongoza ikiwa na alama tatu ikifuatiwa na CR Belouizdad na TP Mazembe kila moja ikiwa na pointi moja, wakati Kundi C Horoya FC ipo kileleni na alama tatu ikifuatiwa na Wydad Casablanca na Kaizer Chiefs ambazo hazicheza huku Petro de Luanda ikiburuza mkia.

Katika Kundi D, ES Tunis ipo kileleni na pointi tatu ikifuatiwa na MC Alger na Zamalek ambazo zina pointi moja moja huku Teungueth ikiburuza mkia bila pointi.

Lakini Al Ahly ni timu pekee hadi sasa iliyoweka rekodi ya kushinda mabao mengi zaidi katika raundi hii ya kwanza huku Simba ikishikilia rekodi ya kuwa timu pekee iliyoshinda ugenini hadi sasa kwenye hatua hii ya makundi.

Ushindi wa Al Ahly juzi, ni salama tosha kwa Simba kujiandaa vizuri, ambayo inatarajiwa kuikaribisha Jumanne ijayo Februari 23 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo ya juzi, Al Ahly inayonolewa na Pitso Mosimane raia wa Afrika Kusini, ilimiliki mpira kwa asilimia kubwa kipindi cha kwanza na cha pili, lakini ilibidi kusubiri hadi dakika ya 57 kupata bao la kwanza kupitia kwa Mohamed Magdy kabla ya dakika sita baadaye Mahmoud Kahraba kutupia la pili na kisha Walter Bwalya kuhitimisha ushindi huo dakika ya 71.

Al Ahly na Simba zitakutana kila moja ikiwa na rekodi ya kushinda nyumbani wakati timu hizo zilipopangwa kundi moja msimu wa 2018/19 na zote zikatinga hatua ya robo fainali wakati huo zikiwa kundi moja na AS Vita na JS Saoura ya Algeria. Mechi ya kwanza Simba ilikubali kichapo cha mabao 5-0 ugenini kabla ya kushinda 1-0 ziliporudiana jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes da Rosa, amesema kwa sasa hesabu zake ni kuvuna kwanza pointi tatu kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma leo.

Gomes amemwambia mwandishi wetu kuwa malengo ya Simba ni kutetea ubingwa wao wa Ligi Kuu Bara na Kombe la FA pamoja na kufanya vizuri kwa kufika mbali kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo anataka pointi tatu kwanza leo kabla ya kuanza hesabu za Al Ahly.

"Mchezo uliopo mbele yetu ni dhidi ya Biashara United tunataka pointi tatu ili kuendelea kuwa kwenye mbio za ubingwa, baada ya hapo ndipo tutageukia hesabu dhidi ya Al Ahly, mechi ambayo najua pia haitakuwa rahisi ila tutapambana," alisema.

## NAMUNGO: WAANGOLA HAWATATOKA CAF DAR

**Na Saada Akida**

BAADA ya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), kutoa taarifa rasmi kuwa mechi zote mbili za mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika kati ya Namungo FC na Clube Desportivo 1º de Agosto ya Angola zitapigwa hapa nchini, uongozi wa klabu hiyo ya Tanzania, umesema watahakikisha Waangola hao wanadondosha pointi zote sita.

Kamati ya Mashindano ya CAF imefikia uamuzi huo baada ya kubaini kuwa si CD de Agosto wala Namungo FC iliyohusika moja kwa moja kukwamisha mechi ya kwanza iliyokuwa ichezwe Februari 14 nchini Angola, hivyo mechi zote mbili zitatakiwa kuchezwa ndani ya saa 72, na ziwe zimechezwa kufikia Februari 26, mwaka huu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ratiba hiyo, CD de Agosto itakuwa mwenyeji wa mechi ya kwanza, ambapo itawajibika katika maandalizi yote ikiwamo gharama za maofisa wa mechi hiyo na kwa kuwa makundi ya Kombe la Shirikisho yatapangwa Februari 22, mwaka huu, mshindi wa jumla baada ya mechi hizo mbili hatazingatiwa katika viwango (non-ranked) wakati wa upangaji.

Mechi ya kwanza nchini Angola iliahirishwa kwa kile kilichoelezwa kuwa mamlaka nchini humo iliwataka wachezaji wote wa Namungo wawekwe karantini baada ya wachezaji watatu pamoja na kiongozi mmoja wa Namungo kuelezwa kuwa wamekutwa na maambukizi ya virusi vya corona ambapo Namungo iligomea uamuzi huo kabla ya kurejea nchini juzi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alisema tayari kwa upande wao wameshapokea taarifa kutoka CAF ambayo inaeleza kuwa mechi zote mbili za kombe hilo dhidi ya CD de Agosto kuchezwa nchini Tanzania.

Alisema kwa taarifa hizo kwao ni faida kwa sababu watakuwa wakicheza mechi zote nyumbani licha ya mechi ya kwanza kucheza kama wageni kwa CD de Agosto kutambulika kama wenyeji wakicheza hapa nchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002